Taarifa ya Sheria za Ulinzi wa Haki

Septemba 2022

THE LEGAL FRAMEWORK
for the Child-Centered Special Education Process

Unganisha kwa Mfumo wa Kisheria

TEA
Texas Education Agency

Unganisha kwa Elimu Maalum ya TEA

Yaliyomo

YALIYOMO **1**

TAARIFA YA SHERIA ZA ULINZI WA HAKI **1**

HAKI ZA WAZAZI WA WATOTO WALIO NA ULEMAVU **1**

SHERIA ZA ULINZI WA HAKI KATIKA ELIMU MAALUM 1
MZAZI MLEZI KAMA MZAZI 1
MZAZI ALIYETEULIWA KUWAKILISHA MTOTO 1
CHILD FIND 2
TAARIFA ILIYOANDIKWA YA MAPEMA 2
IDHINI YA MZAZI 3
TARATIBU WAKATI WA KUWAADHIBU WATOTO WALIO NA ULEMAVU 5
ARIFA 7
JUMLA 7
UWEKAJI WAKATI WA RUFAA 8
UWEKAJI WA HIARI KATIKA SHULE ZA KIBINAFSI NA WAZAZI 11
UHAMISHO WA HAKI ZA MZAZI 11
MAELEZO YA ELIMU MAALUM 12
UTATUZI WA MIGOGORO 12
UWEZESHAJI WA IEP YA JIMBO 13
HUDUMA ZA UPATANISHO 13
MFUMO WA USULUHISHAJI WA MALALAMIKO YA ELIMU MAALUM 14
TARATIBU ZA USIKILIZAJI WA KESI 15
MAELEZO YA MAWASILIANO 23
MAELEZO YA MAWASILIANO YA UTATUZI WA MIGOGORO 23

SPEDTex ni nyenzo nzuri kwa ajili ya familia!

Wasiliana na SPEDTex, Kituo cha Taarifa za Elimu Maalum.

SPEDTEX
Special Education Information Center

www.spedtex.org | 1.855.773.3839

Hakimiliki © 2022. Shirika la Elimu la Texas. Haki Zote Zimehifadhiwa.

Taarifa ya Sheria za Ulinzi wa Haki

Haki za Wazazi wa Watoto Walio na Ulemavu

Sheria ya Elimu kwa Watu Walio na Ulemavu, (**IDEA**) kama ilivyorekebishwa mnamo mwaka wa 2004, inazihitaji shule kuwapa wazazi walio na mtoto aliye na ulemavu taarifa iliyo na maelezo kamili ya sheria za ulinzi wa haki zinazopatikana katika IDEA na kanuni zinazotekelezwa. Hati hii, iliyotolewa na Shirika la Elimu la Texas (**TEA**) inanuia kuafikia mahitaji ya taarifa hii na kuwasaidia wazazi wa watoto walio na ulemavu kuelewa haki zao chini ya IDEA.

Sheria za Ulinzi wa Haki katika Elimu Maalum

Shini ya IDEA, neno *mzazi* linamaanisha mzazi halisi wa mtoto, mzazi aliyepanga mtoto, mzazi mlezi anayeafikia masharti ya jimbo, mlezi, mtu anayelea kwa nafasi ya mzazi halisi au mzazi mlezi ikiwa ni pamoja na babu/bibi, mzazi wa kambo, au mwanafamilia mwingine anayeishi na mtoto, mtu ambaye anajukumika kisheria katika ustawi wa mtoto, au mzazi aliyeteuliwa kuwakilisha mtoto.

Neno *lugha ya asili* likitumika kwa mtu aliye na ufasaha mdogo wa lugha ya Kiingereza linamaanisha lugha ambayo kwa kawaida hutumiwa na mtu huyo. Linapotumika kwa watu ambao hawana uwezo wa kusikia au wanatatizika kusikia, lugha asili ni namna ya mawasiliano ambayo kwa kawaida huwa inatumika na mtu huyu.

Shule inahitajika kukupatia *Taarifa hii ya Sheria za Ulinzi wa Haki* mara moja tu katika mwaka wa shule, ila shule inapaswa kukupatia nakala nyingine ya hati hii: baada ya pendekezo la kwanza au ombi lako la tathmini; baada ya kupokea lalamiko la kwanza la elimu maalum lililowasilishwa na TEA; baada ya kupokea lalamiko la kwanza la usikilizaji wa kesi katika mwaka wa shule; baada ya kufanyika kwa uamuzi wa kuchukua hatua ya kinidhamu ambayo inajumuisha ubadilishaji wa uwekaji; au baada ya ombi lako.

Wewe na shule mnafanya maamuzi kuhusu mpango wa elimu ya mtoto wako kupitia kamati ya usajili, ukaguzi na ufukuzwaji (**ARD**). Kamati ya ARD inabaini iwapo mtoto wako anastahiki elimu maalum na huduma zingine husika. Kamati ya ARD inaunda, inakagua, na kurekebisha mpango wa elimu binafsi wa mtoto wako (**IEP**) na inabaini uwekaji wa kielimu wa mtoto wako. Maelezo zaidi kuhusu wajibu wa kamati ya ARD na IDEA yanapatikana kutoka shuleni mwako katika hati andamani *Mwongozo wa Mzazi kuhusu Mchakato wa Kujiunga, Ukaguzi na Ufukuzwaji* (Kiungo: fw.escapps.net).

Mzazi Mlezi kama Mzazi

Chini ya IDEA, mzazi mlezi anaweza kuchukua nafasi ya mzazi isipokuwa iwapo sheria au kanuni za jimbo zinazuia au isipokuwa majukumu ya kimkataba na huluki la jimbo au eneo yanamzuia mzazi mlezi kuchukua nafasi ya mzazi. Huko Texas, iwapo wewe ni mlezi wa mtoto aliye na ulemavu, unaweza kuchukua nafasi ya mzazi iwapo utakubali kushiriki katika kufanya maamuzi ya elimu maalum na iwapo utakamilisha mpango unaohitajika wa mafunzo kabla ya mkutano unaofuata wa mtoto wa kamati ya ARD, lakini sio baada ya siku ya 90 baada yako kuanza kuchukua nafasi ya mzazi kwa madhumuni ya kufanya maamuzi ya elimu maalum kuhusu mtoto. Baada ya kukamilisha mpango ulioidhinishwa wa mafunzo, sio lazima ushiriki tena mpango wa mafunzo ili kuchukua nafasi ya mzazi wa mtoto yuleyule au kuhudumu kama mzazi au kama mzazi aliyeteuliwa kuwakilisha mtoto mwingine. Iwapo shule itaamua kutokuteua kama mzazi kwa madhumuni ya kufanya maamuzi ya elimu maalum, ni lazima ikupatie taarifa iliyoandikwa ndani ya siku saba za kalenda baada ya tarehe ambayo uamuzi huu umefanywa. Taarifa lazima ieleze sababu za shirika la elimu la eneo (**LEA**) kwa uamuzi huu na ni lazima ikujulishe kuwa unaweza kuwasilisha lalamiko la elimu maalum kwa TEA.

Mzazi Aliyeteuliwa Kuwakilisha Mtoto

Iwapo, baada ya jitihadi nyingi, shule inashindwa kumtambua au kupata mzazi wa mtoto, mzazi mlezi hataki au hana uwezo wa kuchukua jukumu la mzazi, mtoto haishi katika mazingira ya makazi ya malezi, au mtoto hayuko chini ya uangalizi wa jimbo, shule ni lazima iteue mzazi wa kuwakilisha mtoto ili kuchukua nafasi ya mzazi wa mtoto huyu, isipokuwa iwapo mtoto yupo chini ya uangalizi wa

jimbo na korti imeteua mzazi wa kuwakilisha mtoto. Shule ni lazima iteue mzazi wa kuwakilisha kwa kijana asiye na mwangalizi wala makazi kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usaidizi wa Wasio na Makaazi ya McKinney-Vento. Kadiri inavyowezekana baada ya kuteua mzazi wa kuwakilisha kwa mtoto ambaye hana makazi au yupo katika utunzaji wa eneo jingine mbali na nyumbani, shule ni lazima itoe taarifa iliyoandikwa ya uteuzi kwa mfanyaji uamuzi wa elimu ya mtoto na msimamizi wa kesi.
Kwa maelezo zaidi, tembelea Watoto na Vijana Wasio na Makazi (Kiungo: bit.ly/39v6KzG).

Ili kustahiki kuhudumu kama mzazi aliyeteuliwa kuwakilisha mtoto, unapaswa usiwe mfanyakazi wa TEA, shule, au shirika lolote ambalo linahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto, na haupaswi kuwa na maslahi mengine yoyote yanayokinzana na maslahi ya mtoto. Mtu aliyeteuliwa kama mzazi wa kuwakilisha lazima awe na maarifa na ujuzi wa kutosha, awe anataka kuhudumu, afanye maamuzi huru katika ufuataji wa maslahi ya mtoto, ahakikishe kuwa haki za usikilizaji wa kesi za mtoto hazikiukwi, amtembelee mtoto na shule, akague rekodi za kielimu za mtoto, ashauriane na mtu yeyote anayehusika katika elimu ya mtoto, ahudhurie mikutano ya ARD na akamilishe mpango wa mafunzo. Mtu aliyeteuliwa na shule kuchukua majukumu la mzazi wa kuwakilisha ni lazima akamilishe mpango wa mafunzo kabla ya mkutano wa ARD uliopangwa unaofuata lakini sio baada ya siku 90 baada ya tarehe ya uteuzi wa kwanza kama mzazi wa kuwakilisha mtoto. Baada ya kukamilisha mpango ulioidhinishwa wa mafunzo, sio lazima ushiriki tena mpango wa mafunzo ili kuchukua nafasi ya mzazi wa mtoto yuleyule au kuhudumu kama mzazi au kama mzazi aliyeteuliwa kuwakilisha mtoto mwingine.

Kwa masharti zaidi kuhusu wazazi wa kuwakilisha mtoto, tafadhali angalia 19 TAC §89.1047 (kiungo: bit.ly/39B7jIa).

Child Find

Watoto wote walio na ulemavu wanaoishi katika jimbo hili, walio na mahitaji ya elimu maalum na huduma husika, ikiwa ni pamoja na watoto walio na ulemavu ambao hawana makazi au walio chini ya uangalizi wa jimbo na watoto walio na ulemavu wanaohudhuria shule za kibinafsi, bila kujali ukali wa ulemavu wao, ni lazima watambuliwe, watafutwe na watathminiwe. Taratibu hii inaitwa *Child Find*.

Kama sehemu ya shughuli za Child Find, LEA ni lazima ichapishe au itangaze taarifa katika gazeti au vyombo vingine vya habari, au vyote viwili, vilivyo na usambazaji wa kutosha ili kujulisha wazazi kuhusu shughuli ya kutafuta, kutambua, na kutathmini watoto walio na mahitaji ya elimu maalum na huduma husika.

Kwa maelezo kamili kuhusu masharti ya huduma ya Child Find, tafadhali angalia Mfumo wa Kisheria wa Mchakato wa Elimu Maalum Unaozingatia Mtoto (Kiungo: fw.escapps.net).

Taarifa Iliyoandikwa ya Mapema

Una haki ya kupatiwa taarifa iliyoandikwa kuhusu hatua za shule kuhusiana na mahitaji ya mtoto wako ya elimu maalum. Shule ni lazima ikupatie taarifa iliyoandikwa ya mapema katika wakati unaofaa kabla ya kupendekeza uanzishaji au ubadilishaji wa utambulisho, tathmini, au uwekaji wa kielimu wa mtoto wako au elimu ya umma inayofaa na ya bila malipo (**FAPE**) inayotolewa kwa mtoto wako. Pia una haki ya kupokea taarifa iliyoandikwa ya mapema kabla ya shule kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini, au uwekaji wa kielimu wa mtoto wako au FAPE inayotolewa kwa mtoto wako. Shule ni lazima itoe taarifa iliyoandikwa mapema bila kujali kama umekubaliana na mabadiliko au uliomba mabadiliko.

Katika Texas, shule ni lazima ikupatie taarifa iliyoandikwa ya mapema angalau siku tano kabla ya kupendekeza au kukataa hatua isipokuwa kama utakubaliana na kipindi kifupi cha wakati.

Ni lazima shule ijumuishe katika taarifa iliyoandikwa ya mapema: maelezo ya hatua ambazo shule inapendekeza au inakataa kuchukua; maelezo ya sababu shule inapendekeza au kukataa hatua; maelezo ya kila taratibu ya uchunguzi, tathmini, rekodi, au ripoti ambayo shule ilitumia katika kufanya uamuzi wa kupendekeza au kukataa hatua; kauli kuwa uko na ulinzi chini ya sheria za ulinzi wa haki za IDEA; maelezo ya jinsi ya kupata nakala ya *Taarifa ya Sheria za Ulinzi wa Haki*; maelezo ya mawasiliano ya watu au mashirika yanayoweza kukusaidia kuelewa IDEA; maelezo ya chaguo zingine ambazo kamati ya ARD ya mtoto wako ilizingatia na sababu chaguo hizi kukataliwa; na maelezo ya sababu zingine kwa nini shule inapendekeza au inakataa hatua.

Taarifa lazima iandikwe katika lugha inayoeleweka na umma na ni lazima itafsiriwe katika lugha yako ya asili au namna nyingine yoyote ya mawasiliano isipokuwa iwapo haiwezekani kufanya hivyo.

Iwapo lugha yako ya asili au namna nyingine ya mawasiliano sio lugha inayoandikwa, ni lazima shule itafsiri taarifa kwa mdomo au kwa namna nyingine katika lugha yako asili au namna nyingine yoyote ya mawasiliano ili uweze kuielewa. Ni lazima shule iwe na ushahidi ulioandikwa kuwa jambo hili limefanyika.

Iwapo, katika wakati wowote shule itaanza kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako, ubatilishe idhini yako ya huduma, shule ni lazima isitishe utoaji wa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako. Kabla ya kusitisha huduma; hata hivyo, shule ni lazima ikupatie taarifa iliyoandikwa ya mapema kwa angalau siku tano kabla ya kuisha kwa huduma isipokuwa kama utakubaliana na kipindi kifupi cha muda.

Barua Pepe

Mzazi wa mtoto aliye na ulemavu anaweza kuchagua kupokea taarifa zilizoandikwa kupitia barua pepe iwapo shule itawezesha upatikanaji wa chaguo hili.

Idhini ya Mzazi

Ni lazima shule ipate idhini yako kabla ya kufanya mambo fulani. Idhini yako inamaanisha kuwa: umepatiwa taarifa zote zinazohusiana na hatua ambayo ruhusa yako inatafutwa katika lugha yako asili au namna nyingine ya mawasiliano; unaelewa na unakubaliana katika maandishi kwa shughuli ambayo ruhusa yako inatafutwa, na idhini iliyoandikwa inaeleza shughuli na inaorodhesha rekodi zozote ambazo zitatolewa na kwa nani; na kwamba unaelewa kuwa utoaji wa idhini yako ni kwa hiari na unaweza kuiondoa wakati wowote. Iwapo ungependa kubatilisha idhini yako katika utoaji unaoendelea wa elimu maalum na huduma husika, ni lazima ufanye hivyo kupitia maandishi. Iwapo utatoa idhini na kisha kuibatilisha, ubatilishaji wako hautatumika katika tarehe za nyuma.

Shule hii ni lazima iweke nyaraka za juhudi adilifu ili kupata idhini ya mzazi. Rekodi ya hati ni lazima ijumuishe rekodi ya majaribio ya shule ya kupata idhini kama vile rekodi zilizo na maelezo ya kupiga simu, nakala za mawasiliano, na rekodi zilizo na maelezo ya ziara zilizofanywa nyumbani kwako na eneo ulikoajiriwa.

Tathmini ya Kwanza

Kabla ya kufanya tathmini ya kwanza ya mtoto wako ili kutambua iwapo mtoto wako anastahiki kuwa mtoto aliye na ulemavu chini ya IDEA, shule ni lazima ikupatie nakala ya *Taarifa ya Ulinzi wa Haki* na taarifa Iliyoandikwa ya mapema ya tathmini iliyopendekezwa na kupata idhini yako. Ni lazima shule ifanye juhudi adilifu za kupata idhini yako kwa tathmini ya kwanza. Idhini yako ya tathmini ya kwanza haimaanishi kuwa pia umetoa idhini yako kwa shule kuanza kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako. Iwapo mtoto wako yuko chini ya uangalizi wa jimbo na haishi nawe, shule haihitajiki kupata idhini yako iwapo hawawezi kukufikia au iwapo haki zako za uzazi zimesitishwa au kupatiwa mtu mwingine kutokana na amri ya mahakama.

Huduma za Kwanza

Shule yako ni lazima ipate idhini yako kabla ya kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza. Shule ni lazima ifanye juhudi adilifu kupata idhini yako kabla ya kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza. Iwapo hutajibu ombi la kutoa idhini yako kwa mtoto ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au iwapo utakataa kutoa idhini kama hiyo au uibatilishe (uighairi) baadaye idhini yako kwa maandishi, shule yako inaweza kukosa kutumia sheria za ulinzi wa haki (yaani, upatanisho, malalamiko ya usikilizaji wa kesi, mkutano wa usuluhishaji, au usikilizaji wa kesi usio na mapendeleo) ili kufikia makubaliano au uamuzi kuwa elimu maalum na huduma husika zinazopendekezwa na kamati ya ARD ya mtoto wako zinaweza kutolewa bila idhini yako.

Iwapo utakataa kutoa idhini yako ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au iwapo hautajibu ombi la kutoa idhini kama hiyo au uibatilishe (uighairi) baadaye idhini yako kwa maandishi na shule ikose kumpa mtoto wako elimu maalum na huduma husika ambazo idhini yako inatafutwa, shule yako haitakuwa ikikiuka masharti ya kutoa FAPE kwa mtoto wako kwa kukosa kutoa huduma hizi kwa mtoto wako; na haihitajiki kufanya mkutano wa kamati ya ARD au kuunda IEP ya mtoto wako kwa elimu maalum na huduma husika ambazo idhini yako imeombwa.

Iwapo utabatilisha (ughairi) idhini yako kwa maandishi katika wakati wowote baada ya mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, basi shule haitaendelea kutoa huduma kama hizi, lakini ni lazima ikupatie taarifa iliyoandikwa ya mapema, kama ilivyoelezwa chini ya mada ya Taarifa Iliyoandikwa ya Mapema, kabla ya kusitisha uendelezaji wa huduma hizi.

Tathmini Nyingine

Ni lazima shule ipate idhini ya kumfanyia mtoto wako tathmini nyingine isipokuwa kama inaweza kuonyesha kuwa ilichukua hatua adilifu ili kupata idhini yako na umekosa kujibu.

Taratibu za Ubatilishaji – Iwapo mtoto wako amesajiliwa katika shule ya umma au unataka kumsajilisha mtoto wako katika shule ya umma na umekataa kutoa idhini au umekosa kujibu ombi la kutoa idhini kwa tathmini ya kwanza, shule yako inaweza, lakini haihitajiki, kutaka kufanya tathmini ya kwanza wa mtoto wako kwa kutumia upatanisho wa IDEA au malalamiko ya usikilizaji wa kesi, mkutano wa usuluhishaji, na taratibu za usikilizaji wa kesi usio na mapendeleo. Shule yako haitakiuka majukumu yake ya kutafuta, kutambua na kutathmini mtoto wako (jukumu la child find) iwapo haitafuata tathmini ya mtoto wako katika hali hizi.

Iwapo utakataa kutoa idhini ya tathmini nyingine ya mtoto wako, shule inaweza, lakini haihitajiki, kutafuta tathmini nyingine wa mtoto wako kwa kutumia upatanisho, malalamiko ya usikilizaji wa kesi, mkutano wa usuluhishaji, na taratibu za usikilizaji wa kesi usio na mapendeleo ili kutafuta ubatilishaji wa ukataaji wako wa kutoa idhini kwa tathmini nyingine ya mtoto wako. Kulingana na tathmini za kwanza, shule yako haikiuki wajibu wake chini ya IDEA iwapo inakataa kutafuta tathmini nyingine kwa namna hii.

Iwapo mzazi wa mtoto ambaye anasomea nyumbani au amewekwa katika shule ya kibinafsi na wazazi kwa gharama yao hatatoa idhini kwa tathmini ya kwanza au tathmini nyingine au mzazi anakosa kujibu ombi la kutoa idhini, shule inaweza kukosa kutumia idhini ya IDEA kubatilisha taratibu zilizoelezwa hapa juu. Wilaya ya shule haihitajiki pia kuzingatia mtoto wako kuwa anastahiki kupokea huduma za usawa (huduma zinazotolewa kwa baadhi ya watoto walio na ulemavu waliowekwa katika shule za kibinafsi na wazazi).

Idhini yako haihitajiki kabla ya shule kufanya ukaguzi wa data iliyopo kama sehemu ya tathmini au tathmini nyingine au inapompatia mtoto wako mtihani au tathmini nyingine unaotolewa kwa watoto wote isipokuwa iwapo idhini ya mzazi inahitajika kwa watoto wote. Shule inaweza kukosa kutumia ukataaji wako wa kutoa idhini kwa huduma au shughuli moja ili kukunyima wewe au mtoto wako huduma, manufaa au shughuli nyingine.

Tathmini Huru ya Elimu

Tathmini huru ya elimu (**IEE**) ni tathmini inayofanywa na mtu aliyehitimu ambaye si mwajiriwa wa shule. Una haki ya kupata IEE kwa mtoto wako iwapo hutakubaliana na tathmini ya mtoto wako ambayo ilitekelezwa na shule yako. Wakati utaomba IEE, shule ni lazima ikupatie maelezo kuhusu vigezo vyake vya tathmini na mahali pa kupata IEE.

IEE kwa Gharama ya Umma

Iwapo utakosa kukubaliana na tathmini iliyofanywa na shule, una haki ya kuomba mtoto wako afanyiwe tathmini, kwa gharama ya umma, na mtu ambaye si mwajiriwa wa shule.

Gharama ya umma inamaanisha kuwa shule inalipia gharama yote ya tathmini au inahakikisha kuwa tathmini inatolewa kwako bila malipo yoyote.

Iwapo utaomba IEE ya mtoto wako kwa gharama ya umma, shule yako ni lazima, bila kuchelewa kusikofaa, **iweze**: (a) Kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi ili kuomba usikilizaji wa kesi kuonyesha kuwa tathmini ya mtoto wako inafaa; **au** (b) Kutoa IEE kwa gharama ya umma, isipokuwa iwapo shule itaonyesha katika usikilizaji wa kesi kuwa tathmini iliyofanywa kwa mtoto wako haikuafikia vigezo vya shule.

Una haki ya kupata IEE moja pekee kwa gharama ya umma kila wakati shule inapofanya tathmini ambayo unakataa.

Iwapo utaomba IEE ya mtoto wako, shule inaweza kukuuliza ni kwa nini unapinga utathmini huu wa mtoto wako uliofanywa na shule yako. Hata hivyo, shule yako inaweza kukosa kuhitaji ufafanuzi na haipaswi kuchelewesha kusikofaa katika kutoa IEE ya mtoto wako kwa gharama ya umma au katika kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi ili kuomba usikilizaji wa kesi ili kutetea tathmini ya shule ya mtoto wako.

Vigezo vya IEE

Iwapo IEE ni kwa gharama ya umma, vigezo ambavyo tathmini hii itapatikana, ikiwa ni pamoja na eneo la tathmini

na sifa za mtathmini, ni lazima vifanane na vigezo ambavyo shule inatumia inapoanzisha tathmini kwa kiwango ambacho vigezo hivi vinaendana na haki yako ya kupata IEE. Isipokuwa kwa vigezo vinavyotangulia, shule haipaswi kuweka masharti au ratiba ya muda inayohusiana na upataji wa IEE kwa gharama ya umma.

Ubainishaji wa Afisa wa Usikilizaji wa Kesi

Iwapo shule itawasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi ili kuomba usikilizaji wa kesi na afisa wa usikilizaji aamue kuwa tathmini ya shule inapaswa au IEE uliyopata haiafikii vigezo vya IEE vya shule, sio lazima shule ilipie IEE.

IEE kwa Gharama ya Kibinafsi

Wakati wote una haki ya kupata IEE kwa gharama yako. Haijalishi nani anayelipia, shule ni lazima izingatie IEE katika uamuzi wowote kuhusiana na utoaji wa FAPE kwa mtoto wako iwapo IEE inaafikia vigezo vya shule. Pia unaweza kuwasilisha IEE kama ushahidi katika usikilizaji wa kesi.

IEE Inayoagizwa na Afisa wa Usikilizaji wa Kesi

Iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi ataamrisha IEE kama sehemu ya usikilizaji wa kesi, ni lazima shule ilipie.

Taratibu Wakati wa Kuwaadhibu Watoto Walio na Ulemavu

Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule

Ubainishaji Kulingana na Kila Kesi

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatia hali zozote za kipekee kulingana na kila kesi wanapoamua iwapo ubadilishaji wa uwekaji, unaofanywa kulingana na masharti yafuatayo yanayohusiana na nidhamu, yanafaa kwa mtoto aliye na ulemavu ambaye anavunja kanuni za nidhamu za shule.

Jumla

Kwa kiwango kuwa pia watachukua hatua kama hii kwa watoto wasio na ulemavu, wafanyakazi wa shule wanaweza, kwa siku zisizozidi 10 kwa mfululizo, kuondoa mtoto aliye na ulemavu anayekiuka kanuni za nidhamu katika uwekaji wake wa sasa kwa mazingira mbadala yanayofaa ya muda ya kielimu **(IAES)**, mazingira mengine, au kusimamishwa. Wafanyakazi wa shule pia wanaweza kuweka uondoaji zaidi kwa mtoto wa siku zisizozidi 10 za shule kwa mfululizo katika mwaka uleule wa shule katika matukio tofauti ya ukosaji nidhamu, almradi uondoaji huu haujumuishi ubadilishaji wa uwekaji (angalia mada ya Ubadilishaji wa Uwekaji kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu kwa ajili ya ufafanuzi). Pindi tu mtoto aliye na ulemavu anapoondolewa katika uwekaji wake wa sasa kwa jumla ya siku 10 za shule katika mwaka sawa wa shule, shule ni lazima, wakati wa siku zinazofuata za uondoaji katika mwaka huo wa elimu shuleni, itoe huduma kwa kiwango kinachohitajika chini ya Huduma za mada ndogo.

Mamlaka za Ziada

Iwapo tabia inayokiuka kanuni za nidhamu haikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto, na ubadilishaji wa uwekaji utazidi siku 10 za shule kwa mfululizo, wafanyakazi wa shule wanaweza kutumia taratibu za nidhamu kwa mtoto huyu aliye na ulemavu kwa namna sawa na kwa kipindi sawa kama ingekuwa kwa watoto wasio na ulemavu, isipokuwa shule inapaswa kutoa huduma kwa mtoto huyo kama ilivyoelezwa hapo chini katika Huduma. Kamati ya mtoto ya ARD inabaini IAES ya huduma kama hizi.

Huduma

Wilaya ya shule haitoi huduma kwa mtoto aliye na ulemavu au mtoto ambaye hana ulemavu ambaye ameondoewa kutoka uwekaji wake wa sasa kwa siku 10 au chache za shule katika mwaka huo wa elimu.

Mtoto aliye na ulemavu ambaye anaondolewa kutoka kwa uwekaji wa sasa kwa zaidi ya siku 10 za shule na tabia sio udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto au aliyeondolewa chini ya hali maalum ni lazima:

- Aendelee kupokea huduma za kielimu (apate FAPE), ili iwezeshe mtoto aendelee kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, hata ingawa katika mazingira mengine (yanayoweza kuwa ni IAES), na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; na
- Apokee, kama inavyotakikana, tathmini ya tabia inayoendelea, na huduma za uingiliaji wa tabia na urekebishaji, ambazo zimeundwa kushughulikia ukiukwaji wa tabia ili usifanyike tena.

Baada ya mtoto aliye na ulemavu kuondolewa katika uwekaji wake wa sasa kwa siku 10 katika mwaka huohuo wa shule, na iwapo uondoaji huu wa sasa ni wa siku 10 mfululizo au chache na iwapo uondoaji sio ubadilishaji wa uwekaji (angalia ufafanuzi hapo chini), kisha mfanyakazi wa shule,

kwa kushauriana na angalau mwalimu mmoja wa mtoto, atabaini kiwango ambacho huduma zinahitajika ili kuwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine, na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

Iwapo uondoaji ni ubadilishaji wa uwekaji, kamati ya mtoto ya ARD inabaini huduma inayofaa ili kuwezesha mtoto aendelee kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, hata ingawa katika mazingira mengine (ambayo inaweza kuwa ni IAES), na kuendelea katika kufikia malengo yaliyopangwa katika IEP ya mtoto.

Ubainishaji wa Udhihirishaji

Ndani ya siku 10 za shule za uamuzi wowote wa kubadilisha uwekaji wa mtoto aliye na ulemavu kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za nidhamu ya wanafunzi (isipokuwa katika uondoaji ambao ni wa siku 10 mfululizo za shule au chini na sio ubadilishaji wa uwekaji), shule, wewe, na washirika husika wa kamati ya ARD (kama ilivyobainishwa na wewe na shule) mnapaswa kukagua maelezo yoyote yanayofaa katika faili ya mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na IEP ya mtoto, uangalizi wowote wa mwalimu, na maelezo yoyote yanayofaa uliyoyatoa ili kubaini:

- Iwapo tabia iliyokiukwa ilisababishwa na, au ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja au kwa kiwango kikubwa na, ulemavu wa mtoto; au
- Iwapo tabia iliyokiukwa ilisababishwa moja kwa moja na ukosaji wa shule kushindwa kutekeleza IEP ya mtoto.

Iwapo shule, wewe na washirika wanaofaa wa kamati ya ARD watabaini kuwa mojawapo ya hali hizi imeafikiwa, tabia hii ni lazima ibainishwe kuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto.

Iwapo shule, wewe, na washirika wanaofaa wa kamati ya ARD ya mtoto watabaini kuwa tabia iliyokiukwa ilisababishwa moja kwa moja na shule kushindwa kutekeleza IEP, shule ni lazima ichukue hatua ya moja kwa moja kusuluhisha upungufu huu.

Ubainishaji kuwa Tabia ilikuwa Udhihirishaji wa Ulemavu wa Mtoto

Iwapo shule, wewe, na washirika wanaofaa wa kamati ya ARD mtabaini kuwa tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto, kamati ya ARD ni lazima:

- Ifanye tathmini ya tabia inayosaidia, isipokuwa iwapo shule ilifanya tathmini ya tabia inayosaidia kabla ya tabia iliyosababisha ubadilishaji wa uwekaji uliofanyika, na kutekeleza mpango wa uingiliaji wa tabia kwa mtoto; au
- Iwapo mpango wa uingiliaji wa tabia tayari umeundwa, ifanye ukaguzi wa mpango wa uingiliaji wa tabia, na irekebishe, kama inavyohitajika, ili kutatua tabia hii.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapo chini ya sehemu ya Hali Maalum, shule inapaswa irudishe mtoto wako katika uwekaji ambao mtoto wako aliondolewa, isipokuwa iwapo wewe na wilaya mkubaliane ubadilishaji wa uwekaji kama sehemu ya urekebishaji wa mpango wa uingiliaji wa tabia.

Hali Maalum

Iwe au isiwe kwamba tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto wako, wafanyakazi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi kwa IAES (iliyobainishwa na kamati ya ARD ya mtoto wako) kwa siku za shule zisizozidi 45, iwapo mtoto wako:

- Anaenda na silaha (angalia ufafanuzi hapo chini) shuleni au yuko na silaha akiwa shuleni, au majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya TEA au shule;
- Anajua yuko na au anatumia dawa za kulevya (angalia ufafanuzi hapo chini), au anauza au anaomba kuuziwa bidhaa inayodhibitiwa, (angalia ufafanuzi hapo chini), akiwa shuleni, katika majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya TEA au shule; au
- Anasababisha jeraha sugu la mwilini (angalia ufafanuzi hapo chini) kwa mtu mwingine akiwa shuleni, au majengo ya shule, au katika shughuli ya shuleni iliyo chini ya mamlaka ya TEA au shule.

Fafanuzi

Bidhaa zinazodhibitiwa inamaanisha dawa au bidhaa nyingine iliyotambuliwa katika ratiba za I, II, III, IV, au V katika Sehemu ya 202(c) ya Sheria ya Bidhaa Zinazodhibitiwa (21 U.S.C. 812(c)).

Dawa haramu inamaanisha bidhaa inayodhibitiwa, lakini haijumuishi bidhaa inayodhibitiwa ambayo sio haramu kuimiliki au kutumika chini ya uangalizi wa mtaalamu wa huduma za kiafya aliyeidhinishwa au ambayo inamilikiwa kisheria au inatumika chini ya mamlaka nyingine yoyote chini ya Sheria hiyo au chini ya utoaji mwingine wa sheria ya nchi.

Jeraha sugu la mwili lina maana inayotolewa kwa neno jeraha sugu la mwili chini ya aya ya (3) ya kifungu kidogo (h) ya Sehemu ya 1365 ya Mada ya 18, Sheria ya Marekani.

Silaha ina maana inayotolewa kwa neno silaha hatari chini ya aya ya (2) ya kifungu cha kwanza (g) ya Sehemu ya 930 ya Mada ya 18, Kanuni za Marekani

Arifa

Katika tarehe ambapo itafanya maamuzi ya kufanya uondoaji ambao ni ubadilishaji wa uwekaji wa mtoto wako kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za maadili ya wanafunzi, wilaya ya shule ni lazima ikuarifu kuhusu uamuzi huu, na kukupa taarifa ya sheria za ulinzi wa haki.

Ubadilishaji wa Uwekaji kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu

Uondoaji wa mtoto wako aliye na ulemavu kutoka kwa uwekaji wa sasa wa kielimu ni ubadilishaji wa uwekaji iwapo:

- Uondoaji huu ni wa siku zaidi ya 10 kwa mfululizo; au
- Mtoto wako amepata msururu wa uondoaji ambao umekuwa ni mtindo kwa sababu:
    - Jumla ya msururu wa uondoaji ni zaidi ya siku 10 za shule katika mwaka wa shule;
    - Tabia ya mtoto wako inafanana kwa kiasi kikubwa na tabia ya mtoto katika matukio ya hapo awali ambayo yalisababisha msururu wa uondoaji; na
    - Kwa sababu kama hizi za ziada kama vile urefu wa muda wa kila uondoaji, jumla ya wakati mtoto wako ameondolewa, na ukaribu wa uondoaji kutoka kwa mwingine.

Iwe mtindo wa uondoaji unajumuisha ubadilishaji wa uwekaji unaamuliwa kulingana na kesi na shule na, iwapo utapingwa, unapaswa kukaguliwa kupitia mchakato wa usikilizaji wa kesi na kesi ya mahakama.

Ubainishaji wa Mazingira

Kamati ya ARD hubaini IAES ya uondoaji ambao ni ubadilishaji wa uwekaji, na uondoaji katika Mamlaka ya Ziada na sehemu za Hali Maalum.

Ukataji Rufaa

Jumla

Unaweza kuwasilisha malalamiko ya mchakato wa kuomba usikilizaji wa kesi iwapo haukubaliani na:

- Uamuzi wowote unaohusiana na uwekaji uliofanyika chini ya utoaji huu wa nidhamu; au
- Ubainishaji wa udhihirishaji kama ilivyoelezwa hapo juu.

Shule inaweza kuwasilisha malalamiko ya kuomba usikilizaji wa kesi iwapo inaamini kuwa kudumisha uwekaji wa sasa wa mtoto wako unaweza kwa kiasi kikubwa kusababisha jeraha kwa mtoto wako au kwa wengine.

Mamlaka ya Afisa wa Usikilizaji wa Kesi

Afisa wa usikilizaji wa kesi anayeafikia masharti yaliyoelezwa katika sehemu katika Taratibu za Mchakato wa Usikilizaji wa Kesi hapo chini anaweza kufanya usikilizaji wa kesi na kufanya uamuzi. Afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza:

- Kumrudisha mtoto wako aliye na ulemavu katika uwekaji ambapo mtoto wako aliondolewa iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi atabaini kuwa uondoaji ulikiuka masharti yaliyoelezwa chini ya mada ya Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule, au tabia ya mtoto wako ilikuwa ni udhihirisho wa ulemavu wa mtoto wako; au
- Kuamuru ubadilishaji wa uwekaji wa mtoto wako aliye na ulemavu kwa IAES inayofaa kwa siku zisizozidi 45 iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi atabaini kuwa kudumisha uwekaji wa sasa wa mtoto wako unaweza kwa kiasi kikubwa utasababisha jeraha kwa mtoto wako au kwa wengine.

Taratibu hizi za usikilizaji wa kesi zinaweza kurudiwa, iwapo shule inaamini kuwa kumrudisha mtoto wako katika uwekaji halisi kunaweza kwa kiasi kikubwa kusababisha jeraha kwa mtoto wako au kwa wengine.

Kila wakati wewe au shule inawasilisha malalamiko ya mchakato wa kuomba usikilizaji wa kesi kama huu, usikilizaji wa kesi ni lazima ufanyike ambao unaafikia masharti yaliyoelezwa katika sehemu ya Taratibu za Usikilizaji wa Kesi hapo chini, isipokuwa kama vifuatavyo:

- TEA ama shule inapaswa kupangia usikilizaji wa kesi ulioharakishwa, ambao ni lazima ufanyike ndani ya

siku 20 kutoka tarehe ambapo usikilizaji uliombwa na ni lazima usababishe uamuzi ndani ya siku 10 za shule baada ya usikilizaji wa kesi.

- Isipokuwa iwapo wewe na shule mkubaliane kwa maandishi kuondoa mkutano, au kukubaliana kutumia upatanisho, mkutano wa suluhisho ni lazima ufanyike ndani ya siku saba za kalenda baada ya kupokea taarifa ya malalamiko ya usikilizaji wa kesi. Usikilizaji unaweza kuendelea isipokuwa iwapo jambo hili limesuluhishwa hadi pande zote mbili ziridhike ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya usikilizaji wa kesi.
- Jimbo linaweza kuweka masharti tofauti ya usikilizaji wa kesi ulioharakishwa kuliko kama ilivyoweka katika usikilizaji mwingine wa kesi, isipokuwa kwa ratiba za nyakati, masharti haya yanapaswa kufanana na masharti katika hati hii kuhusiana na usikilizaji wa kesi.

Wewe au shule mnaweza kukata rufaa ya uamuzi katika usikilizaji wa kesi ulioharakishwa kwa namna inayofanana na uamuzi katika usikilizaji mwingine wa kesi, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya Mashtaka ya Kiraia, hapo chini.

Uwekaji Wakati wa Rufaa

Wakati ambapo, kama ilivyoelezwa hapo juu, wewe au shule iwasilishe malalamiko ya usikilizaji wa kesi kuhusiana na mambo ya kinidhamu, mtoto wako anapaswa (isipokuwa iwapo wewe na TEA au shule mkubaliane vinginevyo) kubaki katika IAES akisubiri uamuzi wa afisa wa usikilizaji, au hadi kuisha kwa wakati wa kipindi cha uondoaji kama ilivyotolewa kwa na kuelezwa chini ya mada Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule, yoyote inayotokea kwanza.

Ulinzi wa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Elimu Maalum na Huduma Husika

Jumla

Iwapo mtoto wako hajabainishwa kustahiki elimu maalum na huduma husika na anakiuka kanuni za maadili ya wanafunzi, lakini shule ilifahamu (kama ilivyobainishwa hapo chini) kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu kuwa mtoto wako alikuwa ni mtoto aliye na ulemavu, basi mtoto wako anaweza kusisitiza yoyote ya ulinzi ulioelezwa katika taarifa hii.

Msingi wa Ufahamu wa Masuala ya Kinidhamu

Shule yako itachukuliwa kuwa ilifahamu mtoto wako ni mtoto aliye na ulemavu iwapo, kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu:

- Ulionyesha wasiwasi kwa mfanyakazi wa usimamizi au utawala wa shirika linalofaa la kielimu, au kwa mwalimu wa mtoto wako kuwa mtoto wako anahitaji elimu maalum na huduma husika;
- Uliomba tathmini inayohusiana na ustahiki wa elimu maalum na huduma husika chini ya Sehemu ya B ya IDEA; au
- Mwalimu wa mwanafunzi wako au mfanyakazi mwingine wa shule alionyesha wasiwasi mahususi kuhusu mtindo wa tabia iliyoonyeshwa na mtoto wako moja kwa moja kwa msimamizi elimu maalum wa shule au kwa mfanyakazi mwingine wa usimamizi wa shule.

Hali ya kipekee – Shule haitachukuliwa kuwa na ufahamu kama huo iwapo:

- Haujaruhusu tathmini ya mtoto wako au umekataa huduma za elimu maalum; au
- Mtoto wako ametathminiwa na kubainishwa kuwa sio mtoto aliye na ulemavu chini ya Sehemu ya B ya IDEA .

Hali Zinazotumika iwapo Hakuna Msingi wa Ufahamu

Iwapo kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtoto wako, shule haina ufahamu kuwa mtoto wako ni mtoto aliye na ulemavu kama ilivyoelezwa hapo juu katika Msingi wa Ufahamu wa Masuala ya Kinidhamu na Hali ya Kipekee, mtoto wako anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ambazo zinatumika kwa watoto wasio na ulemavu ambao wanajihusisha katika tabia zinazofanana. Hata hivyo, iwapo ombi litafanywa kutaka tathmini ya mtoto wako wakati wa kipindi cha wakati ambapo mtoto wako anachukuliwa hatua za kinidhamu, tathmini ni lazima ufanyike katika namna iliyoharakishwa. Hadi tathmini ikamilike, mtoto wako anabakia katika uwekaji wa kielimu unaobainishwa na mamlaka za shule, ambao unaweza kujumuisha usimamishaji na ufukuzwaji bila huduma za kielimu. Iwapo mtoto wako atabainishwa kuwa mtoto aliye na ulemavu, kwa kuzingatia maelezo kutoka kwa tathmini iliyofanywa na shule na maelezo uliyoyatoa wewe, shule ni lazima itoe elimu maalum na huduma husika kulingana na Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ni pamoja na masharti ya kinidhamu yaliyoelezwa hapo juu.

Pendekezo la na Hatua ya Utekelezaji wa Sheria na Mamlaka za Mahakama

Sehemu ya B ya IDEA:

- Haikatazi shirika kuripoti uhalifu unaofanywa na mtoto aliye na ulemavu kwa mamlaka zinazofaa; au
- Haizuii utekelezaji wa sheria na mamlaka za mahakama za Texas kutekeleza majukumu yao kulingana na matumizi ya sheria za jimbo na nchi kwa hatia zilizofanywa na mtoto aliye na ulemavu.

Usambazaji wa Rekodi

Iwapo shule itaripoti uhalifu iliyofanywa na mtoto aliye na ulemavu, shule:

- Ni lazima ihakikishe kuwa nakala za elimu maalum ya mtoto na rekodi za kinidhamu zimesambazwa ili kuzingatiwa na mamlaka ambazo mashirika yanaripoti uhalifu; na
- Inaweza kusambaza nakala za elimu maalum na rekodi za kinidhamu za mtoto kwa kiwango tu kinachoruhusiwa na Sheria za Haki za Elimu kwa Familia na Faragha (**FERPA**).

Usiri wa Maelezo

Kama ulivyotumika katika sehemu hii:

Uharibifu unamaanisha uharibifu halisi au uondoaji wa vitambulisho vya kibinafsi kutoka kwa maelezo ili maelezo yasiweze kutambulisha mtu binafsi.

Rekodi za Elimuinamaanisha aina ya rekodi zinazoangaziwa katika maelezo ya *rekodi za elimu* kama ilivyolezwa katika Sehemu 99 ya 34 CFR (sheria zinazotekeleza Haki za Elimu za Familia na Faragha ((FERPA) ya 1974, 20 U.S.C. 1232g).

Shirika Linalohusika linamaanisha wilaya yoyote ya shule, shirika, au taasisi inayokusanya, kuhifadhi au kutumia maelezo yanayoweza kutambulisha mtu binafsi au kutoka ambapo maelezo yanatoka, chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

Maelezo Yanayotambulisha Mtu Binafsi ni pamoja na: jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi, au jina la mwanafamilia mwingine; anwani ya mtoto wako; kitambulisho cha kibinafsi kama vile nambari ya Ustawi wa Kijamii; au orodha ya sifa au maelezo mengine ya kibinafsi ambayo yanaweza kuifanya iwezekane kumtambua mtoto wako kwa usahihi adilifu.

Una haki ya kukagua rekodi nzima ya elimu ya mtoto wako ikiwa ni pamoja na sehemu zinazohusiana na elimu maalum. Shule inaweza kuchukulia kuwa una mamlaka ya kuchunguza na kukagua rekodi zinzohusiana na mtoto wako isipokuwa iwapo umeshauriwa kuwa hauna mamlaka chini ya sheria husika za jimbo zinazosimamia masuala kama haya ya ulezi, kutengana na talaka. Pia unaweza kumpa mtu mwingine ruhusa ya kufanya ukaguzi wa rekodi za mtoto wako. Unapoomba kukagua rekodi, shule ni lazima izitoe bila ucheleweshaji usiofaa na kabla ya mkutano wowote kuhusiana na IEP ya mtoto wako, kabla ya usikilizaji wa kesi au kipindi cha usuluhishaji, na sio kwa hali yoyote baada ya siku 45 za kalenda baada ya tarehe ya ombi.

Ufafanuzi, Nakala na Ada

Iwapo utaomba, ni lazima shule ikueleze na ifasiri rekodi, kwa sababu zinazofaa. Ni lazima shule itoe nakala kwa ajili yako iwapo hio ndio njia pekee utaweza kuchunguza na kukagua rekodi. Shule haipaswi kutoza ada za kutafuta au kupata rekodi yoyote ya elimu kuhusu mtoto wako. Hata hivyo, inaweza kutoza ada ya kutoa nakala iwapo hatua ya kutoza ada haitakuzuia kufanya uchunguzi na ukaguzi wa rekodi.

Maelezo ya Zaidi ya Mtoto Mmoja

Iwapo rekodi yoyote ya elimu inajumuisha maelezo ya zaidi ya mtoto mmoja, una haki ya kuchunguza na kukagua maelezo yanayohusiana na mtoto wako pekee au kujua kuhusu maelezo haya mahususi.

Una haki ya kuomba na kupata orodha ya aina na maeneo ya rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa au kutumika na shule.

Idhini ya Kufichua Maelezo Yanayotambulisha Mtu Binafsi

Isipokuwa iwapo maelezo yamo katika rekodi za elimu, na ufichuzi umeidhinishwa bila idhini ya mzazi chini ya FERPA, idhini yako ni lazima ipatikane kabla ya maelezo yanayoweza kutambulisha mtu binafsi yatolewe kwa washirika mbali na mashirika yanayoshiriki. Idhini yako haihitajiki kabla ya maelezo yanayotambulisha mtu binafsi kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kwa malengo ya kuafikia masharti ya Sehemu ya B ya IDEA.

Idhini yako, au idhini ya mtoto anayestahiki ambaye amefika umri wa miaka 18, ni lazima ipatikane kabla ya maelezo ya yanayotambulisha mtu binafsi kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayohusika katika utoaji au ulipiaji wa huduma za mabadiliko.

Iwapo mtoto wako ameandikishwa, au ataandikishwa, katika shule ya kibinafsi ambayo iko eneo tofauti na wilaya ya shule ambako unaishi, idhini yako ni lazima ipatikane kabla ya maelezo yanayotambulisha mtu binafsi kuhusu mtoto kutolewa kati ya maafisa katika wilaya ya shule ambapo shule ya kibinafsi iko na maafisa katika wilaya ya shule ambapo unaishi.

Ni lazima shule iweke kumbukumbu ya kila mtu, isipokuwa kwa ajili yako na maafisa walioidhinishwa wa shule, ambao hukagua rekodi za elimu maalum za mtoto wako, isipokuwa kama ulitoa idhini ya ufichuzi. Kumbukumbu hii ni lazima ihusishe jina la mtu huyu, tarehe ambapo ruhusa ya ufikiaji ilipatikana, na madhumuni ya mtu huyu kuidhinishwa kutumia rekodi hizi.

Afisa mmoja katika shule ni lazima achukue jukumu la kuhakikisha usiri wa maelezo yanayotambulisha mtu binafsi. Watu wote wanaokusanya au kutumia maelezo yanayotambulisha mtu binafsi ni lazima wapokee mafunzo au maelekezo kuhusu sera na taratibu zinazohusiana na usiri chini ya IDEA na FERPA. Kila shule ni lazima idumishe, kwa ajili ya ukaguzi wa umma, orodha ya sasa ya majina na vyeo vya wafanyakazi hawa katika shule ambao wanaweza kufikia maelezo yanayotambulisha mtu binafsi.

Urekebishaji wa Rekodi

Iwapo unaamini kuwa rekodi za mtoto wako sio sahihi, zinapotosha, au zinakiuka haki za mtoto wako, unaweza kuomba shule kurekebisha maelezo haya. Katika wakati unaofaa, shule ni lazima ifanye uamuzi iwapo itarekibisha maelezo haya. Iwapo shule itakataa kufanya marekebisho ya maelezo kama ilivyoombwa, ni lazima ikueleze kuhusu ukataaji huu na haki yako ya usikilizaji wa kesi ili kupinga maelezo katika rekodi hizi. Aina hii ya usikilizaji wa kesi ni kesi ya eneo hili chini ya FERPA na sio mchakato wa usikilizaji wa kesi ya IDEA inayofanywa mbele ya afisa wa usikilizaji wa kesi asiye na mapendeleo.

Iwapo, kutokana na usikilizaji wa kesi, shule inaamua kuwa maelezo haya sio sahihi, yanapotosha, au vinginevyo yanakiuka faragha au haki zingine za mtoto wako, ni lazima ibadilishe maelezo na kukuarifu kwa maandishi. Iwapo, kutokana na usikilizaji wa kesi, shule itaamua kuwa maelezo ni sahihi, hayapotoshi, au vinginevyo hayakiuki faragha au haki zingine za mtoto wako, ni lazima uarifiwe haki yako ya kuweka kauli ya kutoa maoni kuhusu maelezo katika rekodi za mtoto wako kwa muda ambapo rekodi au sehemu inayopingwa inahifadhiwa na shule.

Iwapo utabatilisha idhini yako kwa maandishi kwa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako baada ya shule kutoa huduma mara ya kwanza, shule haihitajiki kurekebisha rekodi za elimu za mtoto wako ili kutoa marejeleo ya huduma za awali la mtoto wako la elimu maalum na huduma husika. Hata hivyo, bado una haki ya kuomba shule irekebishe rekodi za mtoto wako iwapo unaamini rekodi hizi sio sahihi, zinapotosha, au zinakiuka haki za mtoto wako.

Ulinzi na Uharibifu

Shule ni lazima ilinde usiri wa rekodi za mtoto wako katika hatua za ukusanyaji, uhifadhi, ufichuzi na uharibifu. *Uharibifu* unamaanisha uharibifu halisi au uondoaji wa vitambulisho vya kibinafsi kutoka kwa maelezo ili maelezo yasiweze kutambulisha mtu binafsi. Shule ni lazima ikuarifu wakati ambapo maelezo katika rekodi za mtoto wako hayahitajiki ili kutoa huduma za elimu kwa mtoto wako. Maelezo ni lazima yaharibiwe ukiomba yaharibiwe isipokuwa jina, anwani, nambari ya simu, matokeo, rekodi ya mahudhurio, madarasa aliyohudhuria, darasa alilokamilisha na mwaka aliokamilisha.

Taarifa kwa Wazazi

TEA itakupatia taarifa ambayo inatosha kujulisha wazazi kuhusu usiri wa maelezo ya yanayotambulisha mtu binafsi, kiwa ni pamoja na: maelezo ya kiwango cha kutolewa kwa taarifa katika lugha asili za makundi tofauti ya idadi ya watu katika jimbo; maelezo ya watoto ambao maelezo yanayotambulisha mtu binafsi yanahifadhiwa, aina ya maelezo yanayotafutwa, mbinu zitakazotumika katika ukusanyaji maelezo haya, ikiwa ni pamoja na vyanzo ambavyo maelezo yanakusanywa, na matumizi yatakayofanywa na maelezo haya; ufupisho wa sera na taratibu ambazo mashirika yanayohusika ni lazima yafuate kuhusu uhifadhi, ufichuzi kwa watu wengine, uwekaji, na uharibifu wa maelezo yanayotambulisha mtu binafsi; na maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusiana na

maelezo haya, ikiwa ni pamoja na haki chini ya FERPA na sheria za utekelezaji wake katika Sehemu 99 ya 34 CFR .

Uwekaji wa Hiari katika Shule za Kibinafsi na Wazazi

Una haki mahususi wakati ambapo unajitolea kumweka mtoto wako katika shule ya kibinafsi. IDEA haihitaji shule ya umma kulipia gharama za elimu, ikiwa ni pamoja na elimu maalum na huduma husika, kwa mtoto wako aliye na ulemavu katika shule au kituo cha kibinafsi iwapo shule ya umma ilitoa FAPE kwa mtoto wako na unachagua kumweka mtoto wako katika shule au kituo cha kibinafsi. Hata hivyo, shule ya umma ambapo shule ya kibinafsi ipo ni lazima ijumuishe mtoto wako katika idadi ya watu ambao mahitaji yao yanashughulikiwa chini ya sheria za IDEA kuhusuiana na watoto ambao wamewekwa na wazazi wao katika shule ya kibinafsi.

Masharti ya Uwekaji wa Watoto Katika Shule za Kibinafsi Wazazi wa Watoto Katika Shule za Kibinafsi Shule kwa Gharama ya Umma

Una haki mahususi ukimweka mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa sababu haukubaliani na shule ya umma kuhusu upatikanaji wa mipango inayofaa kwa mtoto wako.

Iwapo mtoto wako hapo awali alipokea elimu maalum na huduma husika chini ya mamlaka ya shule ya umma na uliamua kuchagua kumwandikisha mtoto wako katika shule ya chekechea, shule ya msingi, au shule ya upili ua kibinafsi bila idhini ya au pendekezo la shule ya umma, mahakama au afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza kuhitaji shule ya umma kukurejeshea gharama ya uandikishaji iwapo mahakama au afisa wa usikilizaji wa kesi atagundua kuwa shule ya umma haikutoa FAPE kwa mtoto wako kwa wakati unaofaa kabla ya uandikishaji huu na kuwa uwekaji huu katika shule ya kibinafsi unafaa. Afisa wa usikilizaji wa kesi au mahakama inaweza kuamua kuwa uwekaji wako unaofaa hata iwapo uwekaji hauafikii viwango vya jimbo ambavyo vinatumika katika elimu inayotolewa na TEA na shule.

Kikomo cha Urejeshaji

Gharama ya urejeshaji ulioelezwa katika aya inayotangulia inaweza kupunguzwa au kukataliwa iwapo: katika mkutano wa hivi karibuni wa kamati ya ARD ambao ulihudhuria kabla ya kumwondoa mtoto wako kutoka katika shule ya umma, haukuarifu kamati ya ARD kuwa ulikuwa unapinga uwekaji uliopendekezwa na shule ya umma ili kutoa FAPE kwa mtoto wako, ikiwa ni pamoja na kueleza wasiwasi wako na madhumuni yako kutaka kumwandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama ya umma; au kwa angalau siku 10 za kazi, ikiwa ni pamoja na sikukuu ambazo huwa katika siku ya kazi, kabla ya kumwondoa mtoto wako kutoka kwa shule ya umma, haukutoa taarifa iliyoandikwa kwa shule ya umma kuhusu maelezo haya;au, kabla ya kumwondoa mtoto wako kutoka kwa shule ya umma, shule ya umma ilikupatia taarifa iliyoandikwa kabla kuhusu lengo lake la kumtathmini mtoto wako, ikiwa ni pamoja na kauli ya sababu ya malengo ya tathmini ambayo yalifaa na adilifu, lakini haukutoa mtoto afanyiwe tathmini; au mahakama igundue kuwa hatua zako hazikuwa adilifu.

Hata hivyo, gharama ya urejeshaji hazipaswi kupunguzwa au kukatazwa kwa sababu ya kukosa kutoa taarifa iwapo: shule ya umma ilikuzuia kutoa taarifa; haukuwa umepokea taarifa ya jukumu lako la kutoa taarifa iliyoelezwa; au kufuata na masharti yanayotangulia kunaweza kusababisha kujeruhiwa kwa kimwili kwa mtoto wako. Kwa busara ya mahakama au afisa wa usikilizaji wa kesi, gharama ya urejeshaji zinaweza kukosa kupunguzwa au kukatazwa kwa sababu ya umekosa kutoa taarifa inayohitajika iwapo haujui kusoma au kuandika au huwezi kuandika Kiingereza, au kufuata masharti yaliyotanguliwa kunaweza kusababisha athari sugu ya kihisia kwa mtoto wako.

Uhamisho wa Haki za Mzazi

Haki zote za wazazi chini ya uhamisho wa IDEA kwa mtoto wakati ambapo mtoto atafika umri wa kuwa mtu mzima. Umri wa miaka kuwa mtu mzima ni miaka 18 chini ya sheria ya Texas. Kwa watoto wengi, haki zote za mzazi zilizojadiliwa hapo chini katika hati hii zitahamishwa hadi kwa mtoto katika miaka 18 ya umri. Wakati ambapo haki za mzazi zitahamishwa kwa mwanafunzi wako mtu mzima, atakuwa na haki ya kufanya maamuzi ya kielimu, hata ingawa shule ya umma bado itaendelea kukupatia taarifa za mikutano ya kamati ya ARD na taarifa zilizoandikwa za mapema. Wewe, hata hivyo, hupaswi kuhudhuria mikutano isipokuwa iwapo umealikwa mwanafunzi ambaye ni mtu mzima au shule au isipokuwa iwapo mwanafunzi wako aliye mtu mzima anakupatia haki hiyo katika makubaliano baada ya kusaidiwa kufanya uamuzi.

Mlezi Aliyeteuliwa na Mahakama Kwa Mwanafunzi Mtu Mzima

Iwapo mahakama imekuteua au imeteua mtu mwingine kama mlezi wa kisheria wa mwanafunzi mtu mzima, haki chini ya IDEA hazitahamishwa kwa mwanafunzi mtu mzima. Mlezi aliyeteuliwa kisheria atapokea haki hizi.

Mwanafunzi Mtu Mzima Aliyefungwa

Iwapo mwanafunzi mtu mzima amefungwa, haki zote za IDEA zitahamishwa kwa mwanafunzi katika umri wa miaka 18. Hautaweka haki ya kupokea notisi zilizoandikwa hapo awali zinazohusiana na elimu maalum.

Wanafunzi Watu wazima kabla ya Umri wa Miaka 18

Kuna hali fulani zilizoelezwa katika sura 31 ya Sheria ya Familia za Texas ambazo zinasababisha mtoto kuwa mtu mzima kabla ya umri wa miaka 18. Iwapo mtoto wako anabainishwa kuwa mtu mzima katika sura hii, haki chini ya IDEA zitahamishwa kwa mtoto wako katika wakati huu.

Namna Mbadala za Ulezi

Shule ya umma ni lazima iheshimu mamlaka halali ya wakili au makubaliano halali yanayotekelezwa na mtoto wako mzima.

Taarifa ya Maelezo Yanayohitajika

Mnamo au kabla ya mtoto wako kufika umri wa miaka 17, shule ya umma ni lazima ikupatie na mtoto wako taarifa iliyoandikwa kueleza uhamisho wa haki za mzazi na ijumuishe maelezo kuhusu ulezi na namna mbadala za ulezi, ikiwa ni pamoja na makubaliano yanayotokana na usaidizi wa maamuzi, na usaidizi huduma zingine ambazo zinaweza kusaidia mtoto wako kuishi kwa kujitegemea. EIP ya mtoto wako pia ni lazima itaje kuwa shule ya umma ilitoa maelezo haya.

Katika siku ya mtoto wa kuzaliwa ya miaka 18, shule ya umma ni lazima ikupatie wewe na mtoto wako taarifa kuwa haki za mzazi zimehamishwa hadi kwa mwanafunzi mtu mzima. Taarifa hii iliyoandikwa ni lazima ijumuishe maelezo na raslimali kuhusu ulezi na namna njia mbadala za ulezi, ikiwa ni pamoja na makubaliano yanayotokana na usaidizi wa maamuzi, na usaidizi na huduma zingine ambazo zinaweza kusaidia mtoto wako kuishi kwa kujitegemea. Taarifa hii iliyoandikwa ni lazima ijumuishe maelezo ya mawasiliano ya kutumia wakati wa kutafuta maelezo zaidi.

Maelezo ya Elimu Maalum

Iwapo unahitaji maelezo kuhusu masuala ya elimu maalum, unaweza kuwasiliana na Kituo cha Maelezo ya Elimu Maalum katika 1-855-SPEDTEX (1-855-773-3839). Iwapo utapiga nambari hii na kuacha ujumbe mfupi, mtu atakupigia tena simu wakati wa saa za kawaida za kazi. Watu ambao ni viziwi au wana matatizo ya kusikia wanaweza kupiga nambari ya SPEDTEX kwa kutumia huduma ya Relay Texas katika 7-1-1.

Utatuzi wa Migogoro

Kunaweza kuwa na nyakati ambapo hukubaliani na hatua zinazochukuliwa na shule kuhusiana na elimu maalum na huduma husika za mtoto wako. Unahimizwa sana kushirikiana na wafanyakazi wa shule ili kutatua tofauti zinapotokea. Unaweza kuuliza shule kuhusu ni chaguo zinazopatikana kwa wazazi za utatuzi wa migogoro. Iwapo TEA inakupatia chaguo nne rasmi katika kutatua migogoro katika elimu maalum: uwezeshaji wa IEP wa jimbo, huduma za upatanisho, mchakato wa usuluhishaji wa malalamiko ya kielimu, na mpango wa usikilizaji wa kesi.

Tofauti Kati ya Malalamiko ya Usikilizaji wa Kesi na Usikilizaji na Malalamiko ya Elimu Maalum

Sheria za elimu ya maalum za nchi ziliunda taratibu tofauti kwa malalamiko ya elimu maalum na za malalamiko ya usikilizaji wa kesi na usikilizaji. Kama ilivyoelezwa hapo juu, mtu au shirika lolote, ikiwa ni pamoja na lililo nje ya jimbo, linaweza kuwasilisha malalamiko ya elimu maalum ikidai ukiukwaji wa masharti yoyote ya Sehemu ya B ya IDEA na shule, TEA, au shirika lolote la umma. Ni wewe tu au shule inaweza kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi kuhusiana na pendekezo au ukataaji wa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au uwekaji wa kielimu wa mtoto aliye na ulemavu, au utoaji wa FAPE kwa mtoto. Ingawa TEA kwa kawaida inapaswa itatue malalamiko la elimu maalum ndani ya kipindi cha siku 60 za kalenda, isipokuwa iwapo muda wa kipindi hiki utaongezwa kwa wakati unaofaa, na afisa wa usikilizaji wa kesi asiyebagua anapaswa asikilize malalamiko ya usikilizaji wa kesi (iwapo hayakutatuliwa kupitia mkutano wa suluhisho au kupitia upatanisho) na atoe uamuzi ulioandikwa ndani ya siku 45 za kalenda baada ya kumalizika kwa kipindi cha suluhisho, kama ilivyoelezwa katika hati hii chini ya mada Mchakato wa Usuluhishaji, isipokuwa iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi

akubali uongezaji mahususi wa kuda wa kipindi kutokana na ombi lako au ombi la shule.

Uwezeshaji wa IEP ya Jimbo

Kama inavyohitajika na sheria ya jimbo, TEA imeunda mradi wa kuwezesha IEP ili kutoa wawezeshaji huru wa IEP ili kusaidia na mkutano wa kamati ya ARD kwa washirika walio na mgogoro kuhusu maamuzi yanayohusiana na utoaji wa FAPE kwa mtoto aliye na ulemavu. Hali ambazo zinapaswa kuafikiwa kwa TEA ili kutoa mwezeshaji huru ni kama zifuatazo:

- Fomu ya ombi linalohitajika ni lazima ijazwe na kutiwa sahihi na wewe na shule. Fomu hii inapatikana kwa Kiingereza na Kihispania, mtandaoni katika Uwezeshaji wa Mpango wa Elimu Binafsi (Kiungo:/ 3splulV). Pia inapatikana baada ya ombi kutoka kwa TEA.
- Mgogoro huu ni lazima uhusiane na mkutano wa kamati ya ARD ambapo makubaliano ya kuelewana kuhusu moja au zaidi ya vipengele vinavyohitajika vya IEP havikuafikiwa na kamati ya ARD ilikubali kusitisha au kuanzisha tena mkutano huu.
- Wewe na shule ni lazima muwe mumewasilisha fomu ya ombi linalotakikana ndani ya siku 5 za kalenda za mkutano wa kamati ya ARD ulioisha na mgogoro, na mwezeshaji ni lazima awepo katika tarehe iliyowekwa ili kuanzisha mkutano huu tena.
- Mgogoro haufai kuhusiana na ubainishaji wa udhihirisho au ubainishaji wa uwekaji wa IAES.
- Wewe na shule hamfai kuwa wakati huo huo mnahusika katika upatanisho wa elimu maalum.
- Masuala ya mgogoro hayafai kuwa mada ya malalamiko ya elimu maalum au usikilizaji wa kesi wa elimu maalum.
- Wewe na shule hamfai kuwa mmeshiriki katika uwezeshaji wa IEP kuhusiana na mtoto huyu katika mwaka huohuo wa elimu wa uwasilishaji wa ombi la sasa la uwezeshaji wa IEP.
- Sheria ya jimbo linalohusiana na mpango wa uwezeshaji wa IEP ya jimbo inaweza kupatikana katika19 TAC §89.1197 (Kiungo: bit.ly/3bCULCL).

Huduma za Upatanisho

Upatanisho ni lazima upatikane ili kutatua migogoro inayohusiana na suala lolote chini ya Sehemu B ya IDEA, ikiwa ni pamoja na masuala yanayoibuka kabla ya uwasilishaji wa malalamiko ya usikilizaji wa kesi. Kwa hivyo, upatanisho unapatikana ili kusuluhisha migogoro chini ya Sehemu B ya IDEA iwe au la umewasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi ili kuomba usikilizaji wa kesi kama inavyoelezwa chini ya mada Taratibu za Usikilizaji wa Kesi. Upatanisho haujathibitiwa kwa migogoro kati ya wazazi na shule kuhusiana na utambulisho, tathmini au uwekaji wa kielimu wa mtoto au utoaji wa FAPE kwa mtoto huyu.

Upatanisho ni mchakato wa hiari. Kwa hivyo, iwapo wewe na shule mtakubaliana kushiriki katika upatanisho, TEA itafanya mipango na kulipia upatanisho. Upatanisho unaweza kukosa kutumiwa kucheleweshe au kukataza usikilizaji wa kesi unaofaa au haki nyingine chini ya IDEA.

TEA mara moja huwa inatoa huduma za upatanisho kila wakati ombi la usikilizaji wa kesi linapowasilishwa. Lakini, unaweza kuomba huduma za upatanisho wakati wowote wewe na shule mnakuwa hamkubaliani kuhusu suala lolote chini ya Sehemu B ya IDEA.

Wapatanishi sio wafanyakazi wa TEA au wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto ambaye analengwa na mchakato wa upatanisho, na hawawezi kuwa na maslahi yoyote ya kibinafsi au kitaalamu ambayo yanaweza kukinzana na kutopendelea kwao. Mtu ambaye vinginevyo anashtahiki kama mpatanishi sio mfanyakazi wa wilaya ya shule au TEA kwa sababu analipwa na TEA ili kufanya kazi kama mpatanishi. Wapatanishi ni wataalamu ambao wamehitimu na wamefunzwa katika utatuzi wa migogoro na ambao wako na maarifa ya sheria za elimu maalum. Jukumu la mpatanishi ni kuwa na malengo na sio kuegemea upande fulani katika upatanisho. Lengo la upatanisho ni kukusaidia wewe na shule kufikia makubaliano ambayo yanawaridhisha nyote.

Tovuti ya orodha ya sasa ya wapatanishi inaweza kupatikana katika Ofisi ya Ushauri wa Jumla, Mpango wa Upatanisho Maalum (Kiungo:/ 39yQTjK).

Iwapo wewe na shule mtakubaliana kupatanishwa, mnaweza kubaliana kutumia mpatanishi mahususi au mpatanishi atateuliwa kinasibu. Katika kila hali, mpatanishi atawasiliana nawe kwa haraka ili kupanga kipindi cha upatanisho katika mahali na wakati unaofaa kwako na shule.

Majadiliano yanayofanyika katika mchakato wa upatanisho ni lazima yawe siri. Hayapaswi kutumika kama ushahidi katika siku zijazo katika usikilizaji wa kesi au kesi ya kiraia katika mahakama yoyote ya shirikisho au ya jimbo inayopokea usaidizi kutoka kwa Sehemu B ya IDEA.

Iwapo wewe na shule mtatatua mgogoro kupitia mchakato wa upatanisho, pande zote mbili ni lazima ziingie katika makubaliano ya kisheria ambayo yanaanzisha upatanisho huu. Makubaliano ni lazima yataje kuwa majadiliano yote yayolifanyika wakati wa mchakato wa upatanisho yatabaki kuwa siri na hayapaswi kutumika kama ushahidi katika usikilizaji wowote unaofuata wa kesi au kesi ya kiraia. Makubaliano haya yanapaswa pia kutiwa saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye yuko na mamlaka kuidhinisha kwa niaba ya wilaya ya shule. Makubaliano yaliyoandikwa, kutiwa saini yanatambuliwa kisheria na yanaweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ambayo ina mamlaka chini ya sheria ya jimbo ya kusikiliza aina hii ya kesi au katika mahakama ya wilaya ya shirikisho.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu mchakato wa upatanisho katika tovuti ya TEA katika Afisi ya Ushauri wa Jumla, Mpango wa Upatanisho Maalum (Kiungo: bit.ly/39yQTjK).

Sheria ya jimbo inayohusiana na mchakato wa malalamiko ya elimu maalum inaweza ukapatikana katika 19 TAC §89.1193 (Kiungo: bit.ly/35Dyrp2).

Mfumo wa Usuluhishaji wa Malalamiko ya Elimu Maalum

Chaguo lingine la kusuluhisha migogoro ya elimu maalum ni mfumo wa usuluhishaji wa lalamiko wa TEA. Katika hati hii, neno *malalamiko yaelimu maalum* linamaanisha malalamiko kwa jimbo chini ya IDEA na sheria za utekelezaji wake. Iwapo unaamini shirika la umma limekiuka masharti ya elimu maalum, au iwapo unaamini kuwa shirika la umma halitekelezi uamuzi wa usikilizaji wa kesi, unaweza kutuma malalamiko kwa TEA. Pia ni lazima utume malalamiko yako kwa shirika ambalo malalamiko limewekwa dhidi yake wakati mmoja unaotuma malalamiko yako kwa TEA. Shirika au mtu yoyote, ikiwa ni pamoja na kutoka kwa jimbo jingine, anaweza kuwasilisha malalamiko ya elimu maalum na TEA. Kipindi cha malalamiko kitaanza siku inayofuata ya kazi, siku moja baada ya TEA kupokea malalamiko.

TEA imeunda muundo wa fomu ya kusaidia wazazi na washirika wengine katika kuwasilisha malalamiko ya elimu maalum. Upande unaowasilisha malalamiko ya elimu maalum unaweza kutumia muundo huu wa fomu ya jimbo au hati nyingine yoyote almradi malalamiko yanajumuisha maelezo yote yanayohitajika.

Malalamiko yako yaliyoandikwa ni lazima yaeleze ukiukaji uliotokea sio zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ya kupokelewa kwa malalamiko. Malalamiko ni lazima yajumuishe: kauli kuwa shirika la umma limekiuka masharti fulani ya elimu maalum, ukweli ambao kauli hii inatokana, na sahihi na maelezo yako ya mawasiliano. Iwapo malalamiko yanahusu mtoto mahususi, malalamiko haya pia lazima yajumuishe: jina la mtoto na anwani au maelezo yanayopatikana ya mawasiliano iwapo mtoto hana makazi, jina la shule ya mtoto, na maelezo ya hali ya tatizo la mtoto, ikiwa ni pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwako kwa wakati huo. Malalamiko ni lazima yajumuishe upatanisho uliopendekezwa wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa anayelalamika kwa wakati malalamiko yanawasilishwa.

Baada ya kuwasilisha malalamiko ya elimu maalum, TEA itampatia mlalamishi fursa ya kuwasilisha maelezo zaidi kuhusiana na madai ya malalamiko, iwe kwa kunena au maandishi. TEA pia itapatia shirika la umma fursa ya kujibu malalamiko na fursa ya kuwasilisha pendekezo ili kutatua malalamiko haya. Pia, TEA itampatia mzazi aliyewasilisha malalamiko na shirika la umma fursa ya kuhusika katika upatanisho.

Ndani ya siku 60 za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya elimu maalum, TEA itafanya uchunguzi, ikiwa ni pamoja na uchunguzi katika eneo iwapo inahitajika. Kipindi cha siku 60 za kalenda cha kutatua malalamiko kinaweza kuongezwa kwa sababu ya hali za kipekee kwa kuzingatia malalamiko fulani au iwapo pande zote mbili za elimu maalum zitakubaliana kuongeza wakati ili kushiriki katika upatanisho au namna zingine mbadala za utatuzi wa mgogoro.

Katika kufanya uchunguzi, TEA itakagua maelezo yoyote muhimu na kufanya uamuzi huru iwapo shirika la umma limekiuka masharti ya shirikisho au jimbo ya elimu maalum. TEA itatoa uamuzi ulioandikwa ukilenga kila dai ikiwa ni

pamoja na upataji wa ukweli, hitimisho, na sababu za uamuzi wa TEA.
Katika kutatua malalamiko ambapo TEA imebaini kushindwa katika kutoa huduma zinazofaa, TEA ni lazima ishughulikie hai hii ya kushindwa kutoa huduma zinazofaa, ikiwa ni pamoja na hatua za marekebisho zinazofaa ili kushughulikia mahitaji ya mtoto (kama vile huduma za ufidiaji au urejeshaji wa pesa) na utoaji wa huduma unaofaa katika siku zijazo kwa watoto wote walio na ulemavu.

Uamuzi wa TEA kuhusiana na malalamiko ya elimu maalum ni wa mwisho na hauwezi kukatiwa rufaa.

Hatua ya kuwasilisha malalamiko haiondoi haki yako ya kuomba upatanisho au usikilizaji wa kesi. Iwapo utawasilisha malalamiko na kuomba usikilizaji wa kesi kuhusu masuala sawia, TEA itaweka kando masuala yoyote katika malalamiko ambayo yanashughulikiwa katika usikilizaji wa kesi hadi kukamilika kwa usikilizaji. Suala lolote katika malalamiko ambalo sio sehemu ya usikilizaji wa kesi litatatuliwa ndani ya kipindi cha wakati na taratibu zinazoelezwa katika hati hii.

Iwapo suala lililoibuka katika lalamiko linaamuliwa katika usikilizaji wa kesi unaohusisha pande sawa, uamuzi unashughulikia suala hili, na TEA itaarifu mlalamishi kuhusu jambo hili.

TEA ni lazima iwe na taratibu zilizoandikwa za usambazaji mkubwa wa taratibu za malalamiko kwa wazazi na watu wengine walio na maslahi, ikiwa ni pamoja na vituo vya mafunzo na maelezo kwa wazazi, mashirika ya ulinzi na utetezi, vituo vya maisha ya kujitegemea na mashirika mengine yanayofaa.

TEA pia ni lazima iwe na taratibu zilizoandikwa za kuhakikisha utekelezaji ulio na ufanisi wa uamuzi wa mwisho, iwapo itahitajika, ikiwa ni pamoja na: (a) shughuli za usaidizi wa kiufundi; (b) mashauriano; na (c) hatua za marekebisho ili kufikia utiifu.

Unaweza ukapata maelezo zaidi kuhusu mchakato wa malalamiko ya elimu maalum na fomu za uchunguzi wa malalamiko katika tovuti ya TEA katika Michakato ya Usuluhishaji wa Mgogoro wa Elimu Maalum (Kiungo: bit.ly/3bL6n73).

Sheria ya jimbo inayohusiana na mchakato wa upatanisho wa elimu maalum inaweza kupatikana katika 19 TAC §89.1195 (Kiungo: bit.ly/35IU1rY).

Taratibu za Usikilizaji wa Kesi

Chaguo la nne la kutatua migogoro ya elimu maalum ni programu ya usikazaji unoafaa. Katika usikilizaji wa kesi, afisa wa usikilizaji asiyeegemea upande wowote atasikiliza ushahidi kutoka kwa pande zote na kufanya uamuzi unaoshurutisha kisheria.

Ili kuomba usikilizaji wa kesi, wewe au shule (au wakili/mwakilishi wako au wakili/mwakilishi wa shule) ni lazima awasilishe malalamiko ua usikilizaji wa kesi kwa upande mwingine na kuyawasilisha kwa TEA. Una haki ya kuomba usikilizaji wa kesi kwa kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi kuhusiana na suala lolote linalohusiana na utambulisho, tathmini, au uwekaji wa kielimu wa mtoto, au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako.

Iwapo uliwasilisha malalamiko ya mchakato yakinifu mnamo au kabla ya tarehe 31 Agosti, 2022, sheria iliyokuwepo wakati huo ilikutaka uyawasilishe ndani ya mwaka mmoja baada ya tarehe ambayo ulijua au ulipaswa kujua kuhusu madai ya hatua ambayo ndiyo msingi wa malalamiko hayo. Hata hivyo, kwa sababu ya mabadiliko ya sheria, kuanzia tarehe 1 Septemba, 2022, ni lazima uwasilishe malalamiko ya mchakato yakinifu ndani ya miaka miwili baada ya tarehe ambayo ulijua au ulipaswa kujua kuhusu madai ya hatua ambayo ndiyo msingi wa malalamiko hayo. Ratiba hii pia inajulikana kama sheria ya mapungufu. Kipindi hiki hakitumiki kwako iwapo ulizuiwa kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi kwa sababu ya tafsiri zisizo sahihi na shule kwamba ilikuwa imetatua tatizo hili au kwa sababu shule ilikuzuia upate maelezo ambayo yalihitajika upewe. Hata ingawa sio sehemu ya masharti ya IDEA, sheria ya jimbo la Texas inasema kuwa katika hali fulani, sheria ya kikomo cha mwaka mmoja ili kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi kusimamishwa kwa muda au kusimamishwa iwapo wewe ni mshirika wa sasa wa kijeshi, Mfanyakazi wa Kikosi cha Utawala wa Kitaifa wa Bahari na Anga, au Mfanyakazi wa Kikosi cha Huduma ya Afya ya Umma ya Marekani, na iwapo amri ya utoaji wa vidhibiti wa sheria ya shirikisho unaojulikana kama Sheria ya Wanachama ya Usaidizi wa Kiraia, na iwapo sheria ya kikomo ya sheria ya shirikisho

inayojulikana kama Sheria ya Washirika wa Usaidizi wa Kiraia inatumika kwako.

Iwapo utawasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi ili kuomba usikilizaji wa kesi, una jukumu la kuthibitisha kuwa shule ilikiuka masharti ya elimu maalum. Katika hali fulani, shule inaweza kuwasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi ili kuomba usikilizaji wa kesi dhidi yako. Katika hali hizi, shule iko na jukumu la uthibitisho.

Kabla ya kufungulia shule mashtaka katika mahakama kuhusu masuala yoyote yaliyoorodheshwa hapo awali, ni lazima uwasilishe malalamiko ya usikilizaji wa kesi. Iwapo haujafanya hivyo, madai yako yanaweza kutupiliwa mbali katika mahakama.

Uombaji wa Usikilizaji wa Kesi

Wewe au shule hampaswi kuwa na usikilizaji wa kesi hadi wewe au shule (au wakili/mwakilishi wako au wakili/mwakilishi wa shule) mwasilishe malalamiko ya usikilizaji wa kesi yanayojumuisha: jina la mtoto wako na anwani au maelezo ya mawasiliano yanayopatikana iwapo mtoto wako hana makazi; jina la shule ya mtoto wako; maelezo ya tatizo analopitia mtoto wako, ikiwa ni pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo; na suluhisho ya tatizo ambalo unapendekeza kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwako katika wakati huu.

Fomu ya malalamiko ya usikilizaji wa kesi inapatikana kutoka kwa TEA katika Afisi ya Ushauri wa Jumla, Mpango wa Usikilizaji wa Kesi ya Elimu Maalum (Kiungo: bit.ly/2XCdKFw)

Sio lazima utumie fomu ya TEA, lakini malalamiko yako lazima yajumuishe maelezo yanayohitajika hapo juu.

Wewe, wakili wako au mwakilishi wako (au shule, wakili au mwakilishi wake) ni lazima atume malalamiko yaliyoandikwa ya usikilizaji wa kesi kwa TEA na kwa upande unaopinga kwa wakati huohuo. Malalamiko ya usikilizaji wa kesi ni lazima yawekwe kwa siri.

Ili malalamiko ya usikilizaji wa kesi yashughulikiwe, ni lazima yazingatiwe kuwa yanatosha (yameafikia masharti ya yaliyomo hapo juu). Malalamiko a usikilizaji wa kesi yatachukuliwa kuwa yanatosha isipokuwa iwapo upande unaopokea malalamiko ya usikilizaji wa kesi (wewe au shule) utaarifu afisa wa usikilizaji wa kesi na upande mwingine katika maandishi, ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko, kuwa upande unaopokea unaamini kuwa malalamiko ya usikilizaji wa kesi hayaafikii masharti yaliyoorodheshwa hapo juu.

Ndani ya siku tano za kalenda baada ya kupokea taarifa kuwa upande unaopokea (wewe au wilaya ya shule) inazingatia malalamiko ya usikilizaji wa kesi hayatoshi, afisa wa usikilizaji wa kesi lazima aamue iwapo malalamiko ya usikilizaji wa kesi yanaafikia masharti yaliyoorodheshwa hapo juu na kukujulisha wewe na shule kwa maandishi mara moja.

Jibu la Wilaya ya Shule kwa Malalamiko ua Usikilizaji wa Kesi

Iwapo shule bado haijakutumia taarifa iliyoandikwa ya mapema chini ya 34 CFR §300.503 kuhusiana na suala la mada lililopo katika malalamiko ya uikilizaji wa kesi, shule ni lazima, ndani ya siku 10 ya kupokea malalamiko, ikutumie jibu ambalo linajumuisha:

- Fafanuzi la ni kwa nini ilipendekeza au kukataa kuchukua hatua lililoibuka katika malalamiko ya usikilizaji wa kesi;
- Maelezo ya chaguo zingine ambazo kamati ya ARD ilizingatia na sababu ya ni kwa nini chaguo hizo zilikataliwa;
- Maelezo ya kila taratibu ya uchunguzi, tathmini, rekodi, au ripoti iliyotumia kama umsingi wa hatua iliyopendekezwa ua kukataliwa; na
- Ufafanuzi wa sababu zingine ambazo zinahusian na hatua ya shule iliyopendekezwa au kukataliwa.

Hatua ya utoaji wa maelezo haya haitazuia shule kusisitiza kuwa malalamiko yako ya usikilizaji wa kesi hayakutosha, ambapo inafaa.

Jibu la Upande Mwingine kuhusiana na Malalamiko ya Usikilizaji wa Kesi

Isipokuwa kama ilivyotajwa katika sehemu iliyo hapo juu, upande unaopokea malalamiko ya usikilizaji wa kesi lazima, ndani ya siku 10 za kalenda za kupokea lalamiko, utumie upande huo mwingine jibu ambalo linashughulikia masuala yaliyomo katika malalamiko.

Mzazi au shule anaweza kurekebisha au kubadilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi iwapo tu upande mwingine unaidhinisha mabadiliko katika maandishi na unapatiwa fursa ya kutatua malalamiko ya usikilizaji wa kesi kupitia mkutano wa suluhisho au iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi

anatoa ruhusa ndani ya siku za kalenda zisizozidi tano kabla ya usikilizaji kuanza. Upande ambao uliomba usikilizaji unaweza haupaswi kuibua masuala wakati wa usikilizaji ambayo hayakusemwa katika malalamiko ya usikilizaji wa kesi isipokuwa iwapo upande huo mwingine ukubali kuwa masuala zaidi yanaweza kutajwa. Iwapo upande unaowasilisha malalamiko, iwe wewe au shule, utarekebisha (kufanya mabadiliko) kwenye malalamiko ya usikilizaji wa kesi, vipindi vya wakati wa suluhisho na vipindi vya wakati wa kuanza kwa usikilizaji huanza tena katika tarehe ambayo malalamiko yaliyorekebishwa yatawasilishwa.

Ni lazima upatiwe maelezo kuhusu huduma ya bila malipo au ya bei nafuu ya kisheria na huduma zingine husika zinazopatikana katika eneo iwapo utaomba maelezo au iwapo wewe au shule mtawasilisha malalamiko ya usikilizaji wa kesi.

Hali ya Mtoto wakati wa Usikilizaji wa Kesi (Kubaki bila Kuhama)

Isipokuwa kwa usikilizaji wa kesi unaohusisha nidhamu, pindi malalamiko ya usikilizaji wa kesi yanatumwa kwa upande mwingine, wakati wa kipindi cha mchakato wa suluhisho, na huku ukisubiri uamuzi wa usikilizaji wa kesi usioegemea upande wowote au kesi ya mahakama, isipokuwa iwapo wewe na jimbo au shule mkubaliane vinginevyo, mtoto wako atasalia katika uwekaji wa sasa wa kielimu. Kubaki katika hali ya sasa hujulikana kwa kawaida kama kubaki bila kuhama. Iwapo kesi inahusisha nidhamu, angalia Uwekaji Wakati wa Rufaa kwa majadiliano ya uwekaji wa mtoto wakati wa migogoro ya kinidhamu.

Iwapo malalamiko ya usikilizaji wa kesi yanahusisha maombi ili mtoto wako aandikishwe mara ya kwanza katika shule ya umma, mtoto wako ni lazima awekwe, iwapo utaidhinisha, katika mpango wa shule ya umma hadi ukamilishaji wa usikilizaji wa kesi. Iwapo mtoto wako anaenda kufika miaka tatu na anatoka mpango wa Uingiliaji wa Utotoni (**ECI**) programu ya, hali ya kubaki bila kuhama haipo katika huduma za ECI. Iwapo mtoto anastahiki elimu maalum na huduma husika na mzazi atoe idhini, huduma ambazo hazina mgogoro ni lazima zitolewe.

Iwapo afisa wa usikilizaji katika usikilizaji wa kesi unaotekelezwa na TEA anakubaliana nawe kuwa inafaa kubadilisha uwekaji wa mtoto wako, mabadiliko haya katika uwekaji ni lazima yachukuliwe kama makubaliano kati yako na jimbo. Kwa hivyo, mabadiliko haya ya uwekaji yanakuwa uwekaji wa sasa wa mtoto wako ukisubiri matokeo ya rufaa za ziada.

Muda wa Usuluhishaji

Isipokuwa katika kesi ya usikilizaji ulioharakishwa wa kesi, ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko yako ya usikilizaji wa kesi, shule ni lazima ipange mkutano unaoitwa mkutano wa usuluhishaji pamoja na wewe, na mwakilishi wa shule na mamlaka ya ufanyaji maamuzi, na washirika wanaohusika wa kamati ya ARD waliochaguliwa na wewe na shule. Shule yako inapaswa kujumuisha tu wakili katika mkutano iwapo una wakili katika mkutano.

Isipokuwa ambapo wewe na shule mmekubaliana katika maandishi kuondoa mchakato wa usuluhishaji au mmekubaliana kutumia upatanisho badala yake, mkutano wa suluhisho ni lazima ufanyike. Iwapo hautashiriki katika mkutano wa suluhisho, vipindi vya mchakato wa usuluhishaji na usikilizaji vitacheleweshwa hadi mkutano ufanyike.

Iwapo shule itafanya juhudi adilifu ili kukufanya uhudhurie mkutano wa usuluhishaji, lakini ukose kuhudhuria, basi katika mwisho wa kipindi cha siku 30 za kalenda, shule inaweza kuomba afisa wa usikilizaji wa kesi atupilie mbali malalamiko yako. Shule ni lazima iweze kuonyesha kuwa ilifanya juhudi adilifu ili kukufanya uhudhurie mkutano wa usuluhishaji kwa kutumia hati zifuatazo: rekodi ya majaribio ya shule ili kupanga wakati na mahali mlipokubaliana, kama vile rekodi za kina na maelezo ya upigaji wa simu au majaribio ya upigaji na matokeo ya upigaji huu; nakala za mawasiliano zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokelewa; na rekodi za kina za ziara zilizofanywa nyumbani kwako au eneo lako la kazi na matokeo ya ziara hizi.

Iwapo, kwa upande mwingine, shule itashindwa kufanya mkutano wa usuluhishaji ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea taarifa ya malalamiko yako ya usikilizaji wa kesi au akatae kushiriki katika mkutano wa usuluhishaji, unaweza kumwomba afisa wa usikilizaji wa kesi asitishe kipindi cha usuluhishaji na kuamrisha kipindi cha usikilizaji cha siku 45 za kalenda kuanza.

Kwa kawaida, kipindi cha usuluhishaji huwa kinaendelea kwa siku 30 za kalenda. Hata hivyo, iwapo wewe na shule mtakubaliana katika maandishi kusitisha mkutano wa usuluhishaji, basi kipindi cha usikilizaji wa kesi cha siku 45 kitaanza katika siku inayofuata ya kalenda. Vilevile, iwapo wewe na shule mmeanzisha mchakato wa upatanisho au

mkutano wa usuluhishaji, lakini kabla ya mwisho wa kipindi cha usuluhishaji cha siku 30 za kalenda, wewe na shule mkubaliane kwa maandishi kwamba hakuna makubaliano yanayowezekana, basi kipindi cha siku 45 za kalenda kwa usikilizaji kinaanza siku inayofuata ya kalenda. Mwisho, iwapo wewe na shule mmekubaliana kutumia mchakato wa upatanisho, pande zote mbili zinaweza kukubaliana kwa maandishi kuendelea na upatanisho katika mwisho wa muda wa siku 30 za kalenda hadi makubaliano yafanyike. Hata hivyo, iwapo wewe au shule itajiondoa kutoka kwa mchakato wa upatanisho, kipindi cha siku 45 za kalenda cha usikilizaji kitaanza katika siku inayofuata ya kalenda.

Iwapo upande utawasilisha malalamiko yaliyorekebishwa ya usikilizaji wa kesi, vipindi vya muda wa mkutano wa usuluhishaji na kipindi cha wakati wa kusuluhisha malalamiko (kipindi cha usuluhishaji) kinaanza tena wakati malalamiko yaliyorekebishwa ya usikilizaji wa kesi yanapowasilishwa.

Lengo la mkutano wa usuluhishaji ni kukupatia fursa ya kujadili ombi lako na ukweli uliopo na shule na kuipatia shule fursa ya kutatua mgogoro ambao ni msingi wa ombi. Iwapo mtafikia makubaliano, wewe na shule ni lazima mweke makubaliano yenu katika maandishi na kuyatia saini. Makubaliano haya yaliyoandikwa yanaweza kutekelezeka katika mahakama ambayo ina mamlaka chini ya sheria ya jimbo ili kusikiliza aina kama hii ya kesi au katika mahakama ya wilaya ya shirikisho isipokuwa iwapo mhusika mmoja akatae kuhusika katika makubaliano katika siku tatu za kazi kutoka tarehe yaliyotiwa saini.

Iwapo shule haitakuwa imetatua masuala yaliyoibuka katika malalamiko yako ya usikilizaji wa kesi ndani ya siku 30 za kalenda kutoka upokeaji wa malalamiko yako, kipindi cha muda wa siku 45 za kalenda cha usikilizaji wa kesi kitaanza na usikilizaji unaweza kuendelea.

Kipindi cha Usuluhishaji Kilnachoharakishwa

Kwa kipindi kinachoharakishwa cha usikilizaji, shule ni lazima ianzishe mkutano wa usuluhishaji ndani ya siku saba za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya usikilizaji wa kesi. Una haki ya kuwa na usikilizaji wa kesi iwapo shule haijatatua masuala yaliyoibuka katika malalamiko yako hadi uridhike ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko haya. Usikilizaji wa kesi ni lazima ufanyike ndani ya siku 20 za shule kutoka tarehe ambayo malalamiko yaliwasilishwa. Afisa wa usikilizaji wa kesi lazima afanye uamuzi wa mwisho ndani ya siku 10 za shule baada ya usikilizaji wa kesi.

Usikilizaji wa Kesi

TEA inatoa maafisa wa usikilizaji wasioegemea upande wowote ili kufanya usikilizaji. Maafisa wa usikilizaji sio wafanyakazi wa TEA au shirika lolote linalohusika katika elimu au utunzaji wa mtoto wako na hawawezi kuwa na maslahi yoyote ya kibinafsi au kitaalamu ambayo yanaweza kukinzana na upingaji wa usikilizaji. Afisa wa usikilizaji: (1) Anapaswa kuwa na maarifa na kuelewa sheria za IDEA, sheria za shirikisho na jimbo kuhusiana na IDEA, na fafanuzi za kisheria za IDEA na mahakama za shirikisho au jimbo; na (2) Ni lazima awe na maarifa na uwezo wa kuandaa usikilizaji wa kesi, na kufanya na kuandika maamuzi, yanayoendana na yanayofaa desturi za kawaida za kisheria.

TEA inadumisha orodha ya maafisa wa usikilizaji wa kesi inayojumuisha sifa za kuhitimu za kila afisa. Orodha hii inapatikana kwenye tovuti ya TEA katika Afisi ya Ushauri wa Jumla, Usikilizaji wa Kesi za Elimu Maalum (Kiungo: bit.ly/2XCdKFw). Pia unaweza omba orodha hii kutoka kwa Ofisi ya Huduma za Kisheria ya TEA, ambayo maelezo ya mawasiliano yanatolewa katika mwisho wa hati hii.

Kabla ya Usikilizaji wa Kesi

Angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji wa kesi, wewe na shule mnapaswa kufichuliana ushahidi wowote ambao utatolewa katika usikilizaji wa kesi. Upande wowote unaweza kupinga utoaji wa ushahidi wowote ambao haujatolewa kwa wakati. Vivyo hivyo, kwa angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji, wewe na shule ni lazima mfichuliane tathmini zote ambazo zilikamilishwa kabla ya tarehe hii na mapendekezo yanayohusiana na tathmini hizi ambayo wewe au shule mnanuia kutumia katika usikilizaji wa kesi. Afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza kuzuia upande wowote ambao unakosa kufuata masharti haya kutoa tathmini yoyote inayohusiana au pendekezo katika usikilizaji bila idhini ya upande mwingine.

Wakati wa Usikilizaji wa Kesi

Una haki ya kujiwakilisha katika usikilizaji wa kesi. Aidha, upande wowote katika usikilizaji wa kesi (ikiwa ni pamoja na usikilizaji wa kesi inayohusiana na taratibu za kinidhamu) una haki ya:

- Kuandamana ana kushauriwa na wakili na/au watu walio na maarifa maalum au mafunzo mahususi kuhusiana na matatizo ya watoto walio na ulemavu;

- Kujiwakilisha au kuwakilishwa na wakili aliyeidhinishwa na jimbo la Texas au mtu ambaye sio wakili aliyeidhinishwa na jimbo la Texas lakini aliye na maarifa au mafunzo mahususi kuhusiana na matatizo ya watoto walio na ulemavu na ambaye anaafikia sifa zilizotajwa katika 19 TAC §89.1175 (Kiungo: bit.ly/2XFtKq9).
- Kutoa ushahidi na kupinga, kuchunguza kwa undani, na kuhitaji mashahidi kuhudhuria;
- Kuzuia utoaji wa ushahidi wowote katika usikilizaji ambao haujafichuliwa kwa upande huo kwa angalau siku tano kabla ya usikilizaji;
- Kupata rekodi ya usikilizaji iliyoandikwa, au, kwa chaguo lako, ya kielektroniki, ya neno kwa neno; na
- Kupata matokeo yaliyoandikwa, au, kwa chaguo lako, ya kielektroniki.

Haki za Wazazi katika Usikilizaji wa Kesi

Ni lazima uwe na haki ya:

- Kuwa na mtoto wako katika usikilizaji wa kesi;
- Kufungua usikilizaji wa kesi kwa umma; na
- Kuwa na rekodi ya usikilizaji, na matokeo ya ukweli na uamuzi unaotolewa kwako bila malipo yoyote.

Baada ya Usikilizaji wa Kesi

Afisa wa usikilizaji wa kesi atatoa uamuzi. Uamuzi wa afisa wa usikilizaji iwapo mtoto wako alipokea FAPE ni lazima utumie misingi imara. Iwapo utalalamika kuhusu hitilafu ya kitaratibu, afisa wa usikilizaji wa kesi anapaswa kupata tu kuwa mtoto wako hakupokea FAPE iwapo hitilafu hii: Iliathiri haki ya mtoto wako ya kuwa na FAPE; ilinyang'anya mtoto wako manufaa ya kielimu; au iliingilia kati sana fursa yako ya kushiriki katika mfumo wa ufanyaji maamuzi kuhusiana na FAPE kwa mtoto wako. Hakuna sheria zozote zilizoelezwa hapo juu zinaweza kufafanuliwa ili kuzuia afisa wa usikilizaji kuamrisha shule kufuata masharti katika sehemu ya ulinzi wa haki ya sheria ya shirikisho chini ya Sehemu ya B ya IDEA (34 CFR §§500 hadi 300.536).

TEA itahakikisha kuwa uamuzi wa mwisho wa usikilizaji wa kesi umeafikiwa na umetumwa kwa washirika ndani ya siku 45 za kalenda baada ya kumalizika kwa kipindi cha usuluhishaji cha siku 30 za kalenda, au kipindi cha usuluhishaji kilichorekebishwa iwapo kinahusika. Katika usikilizaji unaoharakishwa, TEA itahakikisha kuwa uamuzi wa mwisho umefikiwa ndani ya siku 10 za shule kutoka kwa tarehe ya usikilizaji. Afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza kuruhusu nyongeza mahususi kwa sababu adilifu kutokana na ombi la upande wowote katika usikilizaji usioharakishwa wa kesi. Afisa wa usikilizaji wa kesi hapaswi kuruhusu nyongeza katika usikilizaji unaoharakishwa wa kesi. Uamuzi wa afisa wa usikilizaji wa kesi (ikiwa ni pamoja na uamuzi katika usikilizaji unaohusiana na taratibu za kinidhamu) ni wa mwisho isipokuwa iwapo upande katika usikilizaji (wewe au shule) ukate rufaa kuhusu uamuzi katika mahakama ya jimbo au shirikisho, kama ilivyoelezwa hapo chini.

Ni lazima shule itekeleze uamuzi wa afisa wa usikilizaji wa kesi ndani ya kipindi kilichotajwa na afisa wa usikilizaji, au iwapo hakuna kipindi kilichowekwa, ndani ya siku 10 baada ya tarehe ya kutolewa kwa uamuzi, hata kama shule itakata rufaa juu ya uamuzi, isipokuwa urejeshaji wowote wa pesa za matumizi ya hapo awali unaweza kuzuiwa hadi rufaa isuluhishwe. Hakuna sheria yoyote katika sehemu ya ulinzi wa haki ya sheria za shirikisho chini ya IDEA Sehemu ya B (34 C.F.R. §§300.500 hadi 300.536) inaweza kufasiriwa ili kukuzuia kuwasilisha malalamiko tofauti ya usikilizaji wa kesi kuhusu suala tofauti na usikilizaji wa kesi ambao tayari umewasilishwa

Matokeo ya Uamuzi kwa Jopo la Ushauri na Umma

Baada ya kufuta maelezo yoyote yanayotambulisha mtu binafsi kutoka kwa uamuzi wa afisa wa usikilizaji wa kesi, TEA ni lazima itoe uamuzi (ambao unajumuisha matokeo na maamuzi ya afisa wa usikilizaji) kwa jopo la ushauri la jimbo. Katika Texas, jopo la ushauri la jimbo linaitwa Kamati ya Ushauri Unaoendelezwa. TEA ni lazima pia ifanye uamuzi kupatikana kwa umma.

Mashtaka ya Kiraia

Upande wowote (wewe au shule) ambao haukubaliani na matokeo na uamuzi wa usikilizaji wa kesi (ikiwa ni pamoja na usikilizaji unaohusiana na taratibu za kinidhamu) ana haki ya kukata rufaa matokeo na uamuzi wa afisa wa usikilizaji kwa kufungua mashataka ya kiraia kuhusiana na suala ambalo lilikuwa mada ya usikilizaji wa kesi. Mashtaka yanaweza kufunguliwa katika mahakama ya jimbo ambayo ina mamlaka ya kusikiliza aina kama hii ya kesi au kwa mahakama ya wilaya ya Marekani bila kuzingatia kiwango cha mgogoro na ni lazima iwasilishwe kabla ya kumalizika kwa siku 90 za kalenda baada ya kutolewa kwa uamuzi. Kama sehemu ya mchakato wa ukataji rufaa, mahakama ni lazima ipokee rekodi za usikilizaji wa kesi, isikilize ushahidi wa ziada baada ya ombi la upande wowote, ihusishe uamuzi

wake kutokana na ukubwa wa ushahidi huu, na itoe unafuu wowote unaofaa.

Hakuna kitu chochote katika IDEA kinazuia haki, taratibu, na suluhisho zinazopatikana chini ya Katiba ya Marekani, Sheria ya Wamarekani Walio na Ulemavu ya 1990, Mada V ya Sheria ya Urekebishaji ya 1973 (Sehemu 504), au sheria nyingine za shirikisho zinazolinda haki za watoto walio na ulemavu, isipokuwa kabla ya kufungua mashtaka ya kiraia chini ya sheria hizi katika mahakama kuomba unafuu ambao pia unapatikana chini ya Sehemu ya B ya IDEA, taratibu za usikilizaji wa kesi zinazotolewa chini ya IDEA na kuelezwa hapo juu ni lazima zote zitumike kwa kiwango sawa kama ambavyo ingehitajika iwapo ungefungua mashtaka chini ya Sehemu ya B ya IDEA. Hii inamaanisha kuwa unaweza kuwa suluhisho tayari chini ya sheria zingine ambazo zinaingiliana na zile zinazopatikana chini ya IDEA, lakini kwa jumla, ili kupata nafuu chini ya sheria hizi zingine, ni lazima utumie suluhisho zinazopatikana za usimamizi chini ya IDEA (yaani, malalamiko ya usikilizaji wa kesi; mchakato wa usuluhishaji, ikiwa ni pamoja na mkutano wa usuluhishaji; na taratibu za usikilizaji wa kesi usioegemea upande wowote) kabla ya kufungua mashtaka mahakamani.

Ada za Wakili

Katika mashtaka au kesi yoyote inayoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, mahakama, kwa busara yake, inaweza kutoa ada adilifu kwa wakili kama sehemu ya gharama kwako, iwapo utashinda (shinda).

Katika mashtaka au kesi yoyote inayoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, mahakama inaweza, kwa busara yake, inaweza kutoa ada adilifu kwa wakili kama sehemu ya gharama kwa shule au shirika la elimu la jimbo lililoshinda, ambayo yatalipwa na wakili wako, iwapo wakili: (a) aliwasilisha malalamiko au kesi ya mahakama ambayo mahakama imebaini kuwa isiyo na maana, isiyofaa, au isiyo na msingi; **au** (b) aliendelea kushtaki baada ya mashtaka kuwa yasiyo na maana, yasiyofaa, au bila msingi; **au**

Katika mashtaka au kesi inayoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, mahakama inaweza, kwa busara yake, kutoa ada adilifu kwa wakili kama sehemu ya ada ya shule au shirika la elimu la jimbo linaloshinda, ambazo utalipa wewe au wakili wako, iwapo ombi lako la usikilizaji wa kesi au kesi ya baadaye mahakamani iliwasilishwa kwa sababu isiyofaa, kama vile kunyanyasa, kusababisha uchelewaji usiofaa, au kusababisha ongezeko lisilofaa la gharama ya mashtaka au kesi (usikilizaji).

Mahakama inaamuru ada adilifu za wakili kama ifuatavyo:

- Ada ni lazima zihusishwe na viwango vilivyopo vya kushinda katika jamii ambapo mashtaka au kesi iliibuka kwa aina na ubora wa huduma zilizotolewa. Hakuna bonasi au uzidishaji unapaswa kutumika katika kuhesabu ada zinazoamrishwa.
- Ada hazipaswi kuamrishwa kulipwa na gharama husika hazipaswi kurejeshwa kwa mashtaka au kesi yoyote chini ya Sehemu B ya IDEA kwa huduma zilizotolewa kabla ya ofa iliyoandikwa ya usuluhishaji imetolewa kwako iwapo:
    - Ofa imetolewa ndani ya wakati uliopendekezwa na Sheria 68 ya Sheria za Shirikisho za Utaratibu wa Mashtaka ya Kiraia au, katika hali ya usikilizaji wa kesi, katika wakati wowote wa zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya kuanza kwa usikilizaji;
    - Ofa hii haijakubaliwa ndani ya siku 10 za kalenda; na
    - Mahakama au afisa msimamizi wa usikilizaji wa kesi anagundua kuwa nafuu ambayo tayari ilitolewa kwako haikufai vinavyofaa ikilinganishwa na ofa ya usuluhishaji.

Licha ya vizuizi hivi, amri ya kulipa wakili na gharama husika zinaweza kutolewa kwako iwapo utashinda na ulikuwa na sababu halali kwa kiwango kikubwa katika kukataa ofa ya usuluhishaji.

Ada zinaweza kukosa kuamrishwa kulipwa kuhusiana na mkutano wowote wa kamati ya ARD isipokuwa iwapo mkutano utafanyika kutokana na kesi ya usimamizi au kesi ya mahakama. Mkutano wa usuluhishaji, kama ilivyoelezwa hapo juu, hauzingatiwi kuwa mkutano ulioanzishwa kutokana na usikilizaji wa usimamizi au kesi ya mahakama na hauzingatiwi usikilizaji wa usimamizi au kesi ya mahakama kwa madhumuni ya utoaji wa ada za wakili.

Mahakama inapunguza, kama inavyofaa, kiasi cha ada zinazoamrishwa kulipwa wakili chini ya Sehemu ya B ya IDEA iwapo mahakama itagundua kuwa:

- Wewe au wakili wako, wakati wa uendelezaji wa kesi au usikilizaji, mlichelewesha bila sababu usuluhishaji wa mwisho wa mgogoro;
- Kiasi cha ada za wakili vinginevyo kilichoidhinishwa kutolewa kinazidi kwa kiwango kikubwa kiwango

cha kila saa katika jamii kwa huduma sawa za wakili aliye na ujuzi, sifa na uwezo sawa;
- Wakati uliotumiwa na huduma zilizotolewa zilikuwa nyingi zaidi ikizingatiwa mashtaka au usikilizaji; au
- Wakili anayekuwakilisha hakuipatia shule maelezo yanayofaa katika malalamiko ya usikilizaji wa kesi kama ilivyoelezwa hapo juu katika sehemu ya taratibu za usikilizaji wa kesi.

Hata hivyo, mahakama haipaswi kupunguza ada iwapo itagundua kuwa shule au jimbo lilichelewesha bila sababu suluhisho la mwisho la kesi au usikilizaji au kulikuwa na ukiukaji wa sheria za ulinzi wa haki za Sehemu ya B ya IDEA.

Sheria ya jimbo inayohusiana na mpango wa usikilizaji wa kesi ya elimu maalum inaanza katika 19 TAC §89.1151 (Link: bit.ly/3nQcmtG).

Ukurasa huu uliachwa wazi kimakusudi.

Maelezo ya Mawasiliano

Iwapo una maswali yoyote kuhusu maelezo katika hati hii au unahitaji mtu wa kukuelezea, tafadhali wasiliana na:

Maelezo ya Mawasiliano ya Eneo Hili

Shule:	Kituo cha Huduma za Elimu:	Raslimali Nyingine:
Jina:	Jina:	Jina:
Nambari ya Simu:	Nambari ya Simu:	Nambari ya Simu:
Barua Pepe:	Barua Pepe:	Barua Pepe:

Iwapo unahitaji maelezo kuhusu masuala ya elimu maalum, unaweza kuwasiliana na Kituo cha Maelezo ya Elimu Maalum katika 1-855-SPEDTEX (1-855-773-3839). Iwapo utapiga nambari hii na kuacha ujumbe mfupi, mtu atakupigia tena simu wakati wa saa za kawaida za kazi. Watu ambao ni viziwi au wana matatizo ya kusikia wanaweza kupiga nambari ya SPEDTEX kwa kutumia huduma ya Relay Texas katika 7-1-1.

Iwapo una maswali kuhusu malalamiko yanayosubiri kushughulikia la elimu maalum, tafadhali piga simu nambari 512-463-9414. Iwapo una maswali kuhusu upatanishi au usikilizaji wa kesi unaosubiri kushughulikiwa, wasiliana na mpatanishi au afisa wa usikilizaji wa kesi.

Maelezo ya Mawasiliano ya Utatuzi wa Migogoro

Ukiomba IEP iliyowezeshwa, tuma ombi kwa:	Unapowasilisha Malalamiko ya Elimu Maalum, tuma malalamiko kwa:	Unapoomba Upatanisho, tuma ombi kwa:	Unapowasilisha Malalamiko ya Usikilizaji wa Kesi, tuma lalamiko kwa:
Mradi Wa Uwezeshaji wa IEP ya Jimbo Shirika la Elimu la Texas 1701 N. Congress Avenue Austin, TX 78701-1494 au Faksi: 512-463-9560 au specialeducation@tea.texas.gov	**Kitengo cha Malalamiko ya Elimu Maalum** Shirika la Elimu la Texas 1701 N. Congress Avenue Austin, TX 78701-1494 au Faksi: 512-463-9560 au specialeducation@tea.texas.gov	**Mratibu wa Upatanisho** Shirika la Elimu la Texas 1701 N. Congress Avenue Austin, TX 78701-1494 au Faksi: 512-463-6027 au SE-Legal@tea.texas.gov	**Usikilizaji wa Kesi za Elimu Maalum** Shirika la Elimu la Texas 1701 N. Congress Avenue Austin, TX 78701-1494 au Faksi: 512-463-6027 au SE-Legal@tea.texas.gov

Tafadhali tembelea tovuti ya Idara ya Elimu Maalum katika

https://tea.texas.gov/TexasSped